# MAZUNGUMUZO YA ROHO:

## 1. KUINGIA MU MISA
## 2. MAUNGAMO
## 3. KOMUNYO TAKATIFU

**CENTRE DE LA MISSION ORTHODOKSE**
**KOLWEZI KONGO**
**1996**

**YA PADRI HARALAMBOS VASILOPULOS**

# KITABU YA KWANZA

## JUU YA NINI UNAKATAA KWENDA MU KANISA
## SEHEMU YA KWANZA.

Mimi sijui mambo yako na kanisa. Mara ingine unaenda kila wakati ku kanisa. Mara ingine unabaki mbali ya Kanisa. Mara ingine unaenda ku Kanisa paka siku kuu ya Watakatifu wakubwa. Kwani tuko na Sikukuu na Doksologia ya Watakatifu Wakubwa, na waaminifu wengi wanakuja ku kanisa paka hii Sikukuu. Mara ingine katika juma mingi hauingiake mu Kanisa, kwa sababu unaongojea hapana wakati gani wewe utaenda, lakini wakati gani wao wataenda (wao waaminifu wengine).

Ndugu yangu mupenzi, ninawaza ya kama hii mambo inafanyika, kwani haujue lazima gani na fazila gani uko nayo ku kanisa.

Lakini, nakuomba, fanya nguvu ya kusoma hii kitabu na pasopo mingi mu paka mwisho yake. Mimi sizani ya kama wewe utahitaji sana kufika ku kanisa.

Hausikie watu wengine ao waadui wa Kanisa wanasema, ya kama Kanisa ni nyumba ya Mapadri, huko wanapatikana juu ya kubeba makuta. Hii mawazo yao ni upumbafu. Kama vile kuiko tanuru (four) juu ya kufanya makuta, kwiko hoteli ya kulala wageni, vilevile kuiko na Kanisa, kwani inatusaidia ku lazima yetu ya roho.

Watu wote wa ile wakati walikuwa na hii lazima ya kanisa. Mataifa yote walikuwa na Kanisa, kwa mufano taifa la Wayuda ilikuwa na Kanisa ya Solomono kule muji wa Yerusalema.

Sawa vile tuko na lazima ya maji na pepo juu ya afya (sante) yetu ni vile vile tena tuko na lazima ya Kanisa kwa kumwabudu Mungu na kumuomba.

## SEHEMU YA PILI

1) Katika Kanisa tunasikia ya kama sisi ni watu. Kama mutu mmoja haende ku Kanisa Si mutu? Na huyu hana na macho, na mikono, na miguu, na kichwa? Ndiyo eko na mikono, na miguu na kichwa lakini si mtu. Mambo inaachanisha mtu wasipo miguu na kichwa na ule aliye nayo ni kama anaingia katika Kanisa. Ule mutu anakataa kwenda ku kanisa akili yake ni sawa ya nyama. Ninakuomba, waza juma yote ule mutu anatumika sawa na nyama. Anaamuka pa kitande chake na nyama vilevile anaamuka pa usingizi wake. Kwa mufano, punda. Huyu mtu anakula na nyama anakula vilevile. Huyu mtu anapumzika, nyama anapumzika vilevile. Ule mtu analala na nyama analala vilevile. Halafu, tafauti iko wapi? Tafauti ya hii mambo itaonekana siku ya Mungu. Kama mutu ataenda ku Kanisa kuzungumuza na Mungu Yesu Kristu, hii kazi kila nyama hawezi kuifanya. Ule mutu hapendi kwenda ku Kanisa anasahau ya kama Yeye ni mutu na hali yake inakuwa sawa ya nyama. Anakuwa mukali sawa nyama ya pori. Mwingine anavaa cravate ndevu yake, na anajipakaa manukato ku uso wake, lakini roho yake iko sawa roho ya nyama mukali.
2) Jamii yetu inaendelea mbele? Mambo gani inafika leo katika jamii yetu ? Mambo ya chuki na makelele, majivuno, hakuna uhaki, kazi ya uwongo. Lakini Kanisa iko sawa shamba juu ya kupanda fazila ya ushirika.

Katika Kanisa kuta ya zambi na ya chuki zinaanguka sababu ya sauti ya mahubiri ya Kristu. Watu wote, watajiri na masikini, wakubwa na wadogo, marafiki na maadui wanapatikana wote katika mustari moja.

Wote ni watumishi wa Bwana wao. Wote wanakomunika ku kikombe Takatifu moja. Wanasikiliza Kanisa sawa Mama yao na ni ndugu katika roho na wana nia moja. Ufalme wa mbinguni. Roho inapata ukimya na upole. Ule mutu anatokea ku Kanisa eko zaidi mupole. Anarudia nyumbani mwake na amani rohoni mwake.

Mutajiri mmoja alikuja mara moja mu Kanisa. Alisikia hii neno la Evangeli:
«Mupumbafu wewe! Leo usiku utakufa. Sasa vitu hivi vyote ulivyojitayarishia vitakuwa vya nani? (Luka 12, 20).

Roho yake ilifazaika sana na makelele. Alitamainia kuondoka haraka juu ya kutoka inje ya Kanisa. Juu ya nini ? Kwa sababu jana alinyanganya nyumba ya bibi ya ndugu yake, aliyekuwa mjane. Ku mwisho wa Misa aliendа kumukuta. Akamwambia hivi: «Unihurumia, hii nilikutendea haina haki. Hii nyumba ni yako. Sasa ninakurudisha».

Ndugu ngapi walikuwa wabaya lakini walipoenda mara moja mu Kanisa wakageuza uzima yao?

Katika muji Pireas kule Greece kuliishi mulevi mmoja Baba yake alikufa wakati yeye alikuwa mtoto kidogo na aliacha kwenda ku Kanisa. Tangu umri wa miaka 12 alianza kuiba. Watu wote wakamuchukia. Alifungwa mara nyingi mu udogo. Watu wote wakamuogopa. Analewa, kila mara alizunguka usiku kucha, na akirudi ku nyumba yake alianza kupiga nguvu bibi yake.

Mtu mmoja mwenyi kushona viatu alimwambia aende ku Kanisa. Yeye aliichika. Kule ku Kanisa akaona watu wengi wale alifahamia. Kisha alienda ku Kanisa kila wakati. Aliungama. Akacha kunywa pombe na kufuta tumbako. Makuta yake ilirudia mu nyumba yake.

Aliwashauria watoto wake na alipenda sana watu wote. Mifuko ya mupila yake ilijaa vitabu vya Mungu, na kwa sababu yeye hakujua kusoma aliwapa watu wengine hii vitabu kusoma kwa kupata faita ya roho.

Siku fulani mutumishi mmoja alimupiga, lakini huyu mutu wa Mungu hakupigana. Kabisa wakati wa muchana alienda pamoja naye mu hotel- restaurant, alilipa makuta na walikula pamoja. Watumishi wengine walizungumuza hivi: «Leo tuliona muujiza mmoja. Tuliona kondoo mmoja anapiga imbwa ya pori na huyu imbwa ya pori alikaa kimya. Wale watu wanaenda ku Kanisa weko watu wema kabisa katika inchi. Kwa mufano: mubebe watu 1000 wenyi kuamini na watu 1000 wasipo kuamini. Wingi wa wale watu wenyi kutenda uovu na kuuana ni chache kuliko wenyi kuamini tena ni mingi sana kwa watu wasipo mapendo ya Kanisa.

Neno moja inasem: Tukiotesha majani ndani ya Kanisa (ni kusema watu nawataingiamo), halafu wakifungua buloko na kama wanafungua Kanisa, wanafunga buloko.

3)Tunapata ushindi rohoni mwetu. Apana sisi wote wa Kristu tuko na imani ya nguvu ya kivukutu rohoni mwetu. Kuna wa Kristu wa baridi, wa uzaifu na wa Kristu paka jina tu.

Tuko na lazima ya ninyi juu ya kutoka mu hii baridi ya roho yetu na kupata kivukutu? Shauri. Mukono wa saidio. Fasi takatifu. Halafu Fasi Takatifu ni nyumba ya Mungu na kule kuiko pepo ya roho wa Kanisa na hii pepo itatupatia uzima mpya. Hii mambo tunajua toka maarifa yetu: Kwa zaburi, kwa sala ya Mapadri, ubani na ikone ya Watakatifu hii vitu vyote vinatusaidia, na zaidi sana Liturgia Takatifu. Hii vitu Vitakatifu vyote vinatufungulia njia mpya ku roho yetu. Vinanyanyua na ule muzaifu kupita wengine kisha kunafwata mapendo ya waaminifu, hali ya roho juu ya kulia kwa ajili ya zambi zao na kuomba huruma kwa Mungu. Mara ngapi sisi tulipiga magoti, wakati tuliona watu wengine kufanya hivi? Tena mara ngapi tulirudi ku Kanisa na roho yetu ilikuwa na mawazo mzuri na mupango mpya juu ya kutengeneza mambo ya roho yetu. Iko kweli, ya kama Kanisa inatusaidia sana kwa kuishi yulu ya vitu hivi vya bure vya dunia.

4). Mu juma tunapumuzika:

Watu fulani wa hekima wanasema ya kama na mageuzo ya kazi yetu inaleta nguvu ku mwili na roho zetu. Ni vilevile na watu wakubwa wa siasa. Kisha kazi yao, wanafanya kazi ingine mbalimbali. Lakini kisha wakati fulani, hii mapendo yetu inatusaidia kwa kuingia mu Kanisa. Mapinduzi (Revolution) ya Fransa (France) ilikataza watu kuenda ku Kanisa kwani ilitoka Kristianisme ipite. Waliweka siku ya pumuziko hapana siku ya saba, lakini siku ya kumi. Lakini haikuwezekana. Wakarudisha siku ya pumuziko siku ya juma, kwani nguvu ya mwili aiwezi kutumika siku tisa, paka siku sita. Mungu alijua kuliko wanadamu, na alitayarisha ile siku sita za kazi juu ya watu kutumika, na siku ya saba ni ya kumwabudu Mungu. Kama tunasema siku ya pumuziko, apana kuwaza juu ya kwenda kucheza ku bar na kunywa pombe, ao kulala pasipo kwenda ku Kanisa.

Hata kwacha watu wa jamaa yetu: Watoto ao wagonjwa, kwenda ku mutoni juu ya kunawa, pasipo kusikia kengele juu ya sisi kwenda ku Kanisa. Pumuziko haiko kukaa ndani ya nyumba yetu juu ya kusoma kitabu ya bure, kitabu ile itaweza kuharibu neema ya roho yetu, ao kushimanga Padri ao watu fulani.

Hii matendo yote mubaya inaleta sikitiko ku roho yetu, na inaleta uzaifu ku mwili wetu.

5) Mungu atatulinda. -

Mateso ya uzima wetu, ni mengi majaribu ni mengi. Ewe ndugu yangu, kimbilio lako ni nani ? Utaenda kwa wa kubwa wa l'etat juu ya kukusaidia? Lakini wao hawakusopoke, ao awawazi kukusaidia kwa sababu wao wanangalia paka kazi yao na makuta yao.

Inapashwa kukimbilia ku Kanisa sawa chombo chenye kukimbilia ku kikavu kwa kuepuka zoruba yenyi kutafuta kuingiza chombo ndani ya maji. Mtakatifu Yoane Krisostome anasema hivi: «Mungu alijenga ma Kanisa yake mengi ku fasi mbalimbali, ndio kikavu sababu kuondoa ubaya na sikitiko mu uzima wetu na kuleta amani na utulivu. Ndugu yangu Kanisa itakupatia nguvu sababu ya kushindana na majaribu ya uzima wako.

Bwana Yesu atakupatia neema yake ya kutembea muzuri, kutunza magonjwa ya mwili na roho yako, na atakuchunga kwa kila hatari.

Wakati wa mfalme Theodosios mfalme mkubwa wa muji Konstantinopoli, mtoto mmoja jina lake Theophile, aliuzisha mwili wake sawa mutumwa juu ya baba yake kuishi. Mara ngapi mapendo yake iko mengi kupita. Baba yake alimushauria hivi: «Mtoto yangu kama una kazi mengi, mbele ya kwanza inapashwa kwenda siku ya Mungu mu Kanisa. Utasikiliza neno la Mungu, kiisha Liturgia, utaenda ku kazi yako».

Ule mukubwa wa inchi jina lake Constantino alimuuza, alimupenda sana juu ya fazila yake, na aliishi naye kwake. Siku moja huyu mukubwa aliendа ku nyumba ya Mfalme, akasahahu barua yake ya lazima ndani ya nyumba yake, alimwambia Theophile amuletee ile barua.

Huyu akaenda mu nyumba ya Bwana wake, akakuta bibi ya bwana wake eko nafanya usharati na mutumwa mmoja. Huyu mwanamuke mukalamushi akatayarisha mambo ya uwongo juu Theophile asiseme kwa mume wake.

Akasema: «Huyu Mutumwa Theophile anayetembea pamoja na wewe; alifika ndani ya nyumba na alipenda kufanya usharati na mimi, lakini mutumwa mmoja alinisaidia na alimufukuza Theophile, ndio maana nataka huyu Theophile, umuuwe, kama apana, mimi nitarudi kwa baba yangu.

Bwana yake akasadiki, na alikamata mupango ya kukata kichwa cha Theophile. Alizungumuza na ule mukubwa anangalia mambo ya baraza ya hukuma na kuuwa

akamwambia, kama unaisha hii kazi, utanitumia kichwa cha Theophile ndani ya mufuko. Wakasikilizana hivi kufanya hii mambo siku ya kesho.

Ile siku mukubwa wa Konstantinopoli akamwambia Theophile: «Kwenda kwa mukubwa fulani ukamusalimie kwa ajili yangu, na yeye atakupatia hii jibu ni naongojea». Theophile pasipo kuwa na mawazo mengine, alienda kwa ule mukubwa.

Pa yeye kwenda, Theophile aliona kwa hii njia Kanisa moja; Theophile akaenda huko na akaingia. Na alikaa humo mpaka mwisho wa ibada. Lakini huyu mutumwa alifanya usharati alisikitika kwa sababu hakuona wale watu wataleta kichwa cha Theophile.

Kisha akamwambia bwana wake Konstantino: «Bwana nitaenda mimi juu yakubeba kichwa cha Theophile? Bwana wake akamujibu, kwenda. Akaenda mbio mbio ku nyumba ya ule mukubwa, na akamusalimia kwa jina la Bwana wake Konstantino. Mara moja, askari akapewa ruhusa ya kukata kichwa cha Theophile, alinyanyua mupanga wake na akakata kichwa cha ule mutumwa; na aliwaza ya kama alikata kichwa cha Theophile.

Wakaweka kichwa ndani ya mufuko, na mara moja Theophile akafika na kusalimia ule rafiki ya bwana wake kwa jina la Konstantino. Huyu mukubwa akatosha mufuko akamupa Theophile, huyu pasipo kujua nini iko ndani. Wakati Konstantino alimuona Theophile, akamuuliza unaleta nini ndani ya hii mufuko? Yeye akasema: Rafiki yako analeta juu ya kukupatia wewe, mimi sijue nini iko ndani ya mufuko. Bwana wake alishangaa wakati alipoona hii ukweli, na akamuchukua huyu Theophile sawa mtoto yake wa kweli. Sisi tunaona wakati Theophile aliingia mu Misa aliokoa uzima wake. Mtakatifu Yoano Krisostomo anasema: Ndugu zangu, muje mu Kanisa kupokea baraka ya Mungu na furaha ya roho. Kuja mbele bunduki ya roho juu ya kufukuza shetani».

Mtungaji mmoja wa shairi anasema: ule mtu anaenda na anaingia mu Kanisa akitoka akirudi kwenda kwake, harufu nzuri inatoka pa mwili yake. Kwa sababu Bwana Yesu eko karibu naye.

Ule mtu anaenda mu Kanisa baraka ya Mungu inamubariki, na kazi yake inaendelea muzuri.

Mfanye biashara mmoja alimuuliza fundi mmoja: «Juu ya nini unatumika hii siku ya Mungu? » Huyu akajibu: «Kwa sababu mimi ni masikini». Akamuuliza tena: «Miaka ngapi unatumika? » Yeye akasema: katika miaka yote ya uzima wangu. Lakini mimi sijakua mutajiri» Mfanya biashara akamuambia: «Mimi nakushauria usitumike siku ya Mungu (Dimanche). Utatumika siku sita, kufika siku ya Mungu utaenda ku kanisa.

Na kisha miezi sita, mimi takulipa ile makuta utapoteza katika zile siku haukutumike. Kisha miezi sita huyu mfanya biashara ule mtumishi alimuuliza: «Makuta ngapi unapoteza? Yeye alimujibu:
Sipoteze hata kidogo. Kabisa kabisa ninauza ngombe moja. Halafu mtu mmoja alikua na haki alisema: Najua namna mbili ya mtu kuwa masilini;

Namna ya kwanza ni kama yule mtu anaiba. Namna ya pili ni kama anatumika siku ya Mungu (dimanche). Sawa vile sisi tunasaidia na tunalinda wa ndugu wa nyumba yetu vilevile na Mungu anamulinda na anasaidia yule mtu anapenda kunigia mu Kanisa yake.

6) <u>Kuna Amri za Mungu</u>

Amri ine katika zile kumi za Agano la Kale zinatuonyesha hivi:
Kumbuka siku ya sabato (siku ya Mungu) na uitakase.
Katika zaburi Nabii Daudi anandika hivi; Tukuzeni Mungu katika Kanisa. Mungu alimwambia Nabii Musa kwa ile wakati wa Agano la Kale kufanya ao kutengeneza hema ya ushuhuda, ni kusema fasi ya kumuabudu Mungu, tena Mungu alimwambia Nabii Musa namna gani atatengeneza hii fasi, na kazi ya Mapadri, na vitu ntakatifu. Tena katika Agano Jipya tunaona Bwana Yesu Kristu aliingia mu hekalu ya Salomono kufanya sala

na fundisho pamoja na waebrania. Mitume pamoja na waaminifu wao waliingia mu Kanisa: «Wakaendelea kufundishwa na Mitume, na kuishi katika ushirika, na kumega mukate na kuomba». Philosophe Yustinos aliyeishi miaka mia moja kiisha, shahidi anatuhakikisha ya kama: Kila siku ya Mungu wa Kristiani walienda mu Kanisa. Walisoma sehemu moja Kitabu cha Matendo ya Mitume na Evangelion ao fundisho ya Manabii, Mkubwa wao aliwashauria kila mara kwa kufwata mwenendo wa Watakatifu. Kiisha wote walisimama na kufanya sala kwa Mungu. Kisha sala, mukate na vinyo na maji vilitolewa na Padri anafanya sala, waaminifu watasema:  Amina.

Mwisho, wote walkomunika. Kama wengine ni wagonjwa Mashemasi watawapelekea mwili na damu ya Bwana wetu Yesu Kristu ku manyumba yao».

Tena Kanisa yetu inaleta malipizi kwa yule mwaaminifu anakataa kufwata hii amri ya Mungu, na hatake kwenda ku kanisa juma tatu ya kufwatana. Ni kusema kanuni 170 ya Ikumeniki ya sita inatwambia hivi: «Kama mtu fulani, pasipo mambo ya nguvu, anakataa kwenda ku misa juma tatu, kama yeye ni cleriki, Padri Shemasi inapashwa ku mufinga, kama ni laic inapashwa kumukataza ku Komunika. Halafu sisi tutafanya je? Tutavunja hii amri ya Mungu ?

7) Tunamaliza kazi ya roho yetu;

Ni nini iko kazi yetu ? Kazi yetu ni kumupenda na kumwabudu Mungu! Hii kazi ya kuabudu ni kazi ya Malaika. Na sisi kama tunasikia ao apana, inapashwa kuishi sawa Malaika. Mutu anaweza kupata furaha yake kama anaabudu Mungu na atasikia furaha ya kupita kabisa kama anaabudu Mungu kweli, kwa hivi katika hii mambo inafanyika na muziki, ni kusema kama mtu mmoja anajua kazi kuimba muziki anafurahi sana. Tena na wa nyama ya pori kama wanasikia muziki wanapata amani na furaha; sisi kama tunasikia mwimbo tunasikia furaha kupita wa nyama ya pori. Na wale Watawa wanaishi zamani na sasa katika jangwa ao ma nyumba ya ku kilima na sala ao na Kwarezima wanasikia furaha mingi kwa sababu waliweka uzima wao mikononi mwa Mungu na walipata njia ya kweli na furaha ya kweli.

Sisi wote tunapenda kwenda ao kuishi mu uzima wa milele. Namna gani tunaingia mu ufalme wa Mungu? Kama tunaingia ku muabudu Mungu mu Kanisa na kupata furaha ya kweli. Kama mtu mmoja anakataa kwenda ku masomo kufunza, namna gani ataweza kuingia Universite na ku furahi ? Mu uzima wa milele mutaingia wale watu wenye kuingia mu Kanisa.

Wale wanakataa kuingia mu Kanisa kisha lufu yao,  watatubu, lakini hakuna ule ataweza kusaidia roho yao. Wakati ya kutubu imekwisha kupita.

8) Mu Kanisa, Mungu anatusikia kuliko fasi ingine.

Watu wengi wanasema; Ninafanya sala mingi nyumbani mwangu. Lakini nyumba iko fasi ingine, na Kanisa ni fasi ingine.

Ndani ya nyumba utaweza kufanya sala lakini hautaweza kufanya Liturgia na fumbo ya Komunyo Takatifu. Katika Agano la Kale Mungu anasema: «Pasopo apana kutoa zawadi yako fasi ingine paka kwa hii fasi Bwana Mungu anachagua». Bwana Wetu Yesu Kristu anakaa mu Kanisa. Bwana Yesu anasema: «Pahali watu wa wili ao wa tatu wanaokusanyika kwa ajili yangu mimi niko pale pamoja nao».

Ndugu zangu, wazeni kama Yesu Kristo eko katikati ya watu wa wili ao wa tatu, mara ngapi Kristo atafurahi kama ndani ya Kanisa muko watu wengi.

Ndani ya Kanisa sisi tunaishi sawa jamaa moja ya Bwana wetu Yesu Kristu, kama sisi tunapokea Mwili moja na Damu moja ya Bwana wetu Yesu Kristu. Tunapokea sisi wote uzima wa Kristu ndani yetu na tunaishi sawa ndugu. Kama tuko wengi na tukiomba Mungu anasikiliza wepesi maombi yetu. Kwa mufano: Baba mmoja atatimiza maneno ya watoto wake wote kuliko neno la mtoto mmoja ao wa wili.

Namna moja katika inchi, kama watu wengi wanaomba kitu kwa l'Etat, wakubwa wa inchi watasikia mbio-mbio, kuliko maombi ya watu wachache.

Ndio vile shetani anasikitika kama watu wengi wanaingia mu Kanisa vile shetani anapenda kuwatosha mu Kanisa. Kama kwiko vita. Maadui wanarenda kufunga njia sababu wakubwa wa inchi wasilete ma bunduki juu ya kukataza ile vita. Mtakatifu mmoja wa wakati fulani alipita karibu ya Kanisa moja, na aliona yulu ya Kanisa shetani mwenye kulala.

Ilikuwa siku ya Mungu asubui. Aliendelea na safari yake na akaingia mu hii mugini. Wa Kristu walienda ku Kanisa na wengi walikuwa ndani. Kule aliona mashetani walikaa pembeni ya Kanisa na silaha zao.

Huyu Mtakatifu akamuuliza shetani: «Mambo gani ninyi munakusanyika hapa. Na hapa Kanisa iko na kule nilipita kuko kanisa, sasa namna gani muko wengi hapa lakini kule kuko paka shetani moja? Shetani akamujibu: Angalia ile Kanisa unaona wewe kwiko shetani moja hakwenda wa Kristiani wengi, lakini hapa sawa vile unaona, tuko na kazi mingi…. . »

Tuko na faida mingi ya roho kama tunaingia mu Kanisa, sasa juu ya nini tunakataa?

## SEHEMU YA TATU

### MAMBO YA KUVAA

1) Manguo:

Wengine wanasema ninataka kwenda ku misa lakini namna gani nitaenda na manguo mubaya? Ewe ndugu yangu, kama uko na manguo muzuri utaenda? Kama utaenda, utaenda kufanya sala ao juu ya kuonyesha manguo yako kwa wengine ?

Fasi gani Evangelion ya Kristo inakwambia ya kama wewe unapashwa kwenda ku Kanisa, paka unavaa manguo mpya?

Yesu Kristo ataangalia na nguo yako ao mapenzi yako ya kuomba ao ya kumuabudu Mungu. Basi, kizuio juu kukosa kwenda ku kanisa apana manguo lakini ni roho yako mubaya. Kwiko namna wewe kuniuliza: «Wale watu wataniona watasema nini ? «Mimi nitakujibu; Wewe utangalia watu ao Mungu ?

Watu hawajuwe kabila yako na hali ya uzima yako? Hawakuonake inje ya Kanisa kama hii manguo unavaa iko muzuri ao apana ? Uko na manguo ao hauna nayo ?

Unapashwa kujua kama hauna na manguo ya muzuri lakini uko na unyenyekevu, unazarau mashimango ya watu na unaenda kwa Mungu kuomba, utapata malipo ya roho.

2) WATUMISHI WA KANISA:

Watu wengine wanakataa kuingia mu Kanisa kwa sababu hawafurahi kwa sababu mapadri, waimbaji na wa memba (membres) wa Comite pamoja na wa Kristiani wengine wanafanya vitu vibaya, ni vile wao wanawaza.

Lakini ewe ndugu yangu, juu ya nini unaenda mu Kanisa ? Juu ya kwangalia watu ao kuomba Mungu? Kama watu wengine ni wabaya ao wazuri, hii si mambo yako. Kazi yako ni kwangalia mambo ya uzima yako, juu ya kupokea baraka ya Mungu. Mpenzi wangu, kama Mapadri weko wabaya ao wazuri, Mungu atawahukumu. Na kama wao ni wabaya lakini ni Watumishi wa Mungu, wanatimiza Mafumbo ya Mungu.

Mungu aliwaweka kwa hii kazi juu ya Mungu, utakaso na baraka yake. Kama Mfalme mmoja anakwita mu nyumba yake juu ya kukupa kitu, wewe utakataa kwenda kwa sababu ule mutu Mtumishi wa mfalme ni mubaya? Mupenzi wangu, hawende mu Kanisa juu ya mapadri ao juu ya kwangalia watu wa Comite, lakini unaenda juu ya Bwana Yesu Kristu ili upokee ku mikono ya Padri baraka ya Bwana Yesu Kristu. Kama Padri mmoja ni mwenye zambi, hii haina kizuio juu ya kupoteza neema ya Mungu ku

mikono ya watu. Kwa mufano: kma Mwuaji ao mtoto anakupatia ua (rose de fleur) wewe utaweza kupoteza harufu ya ile ua ? Ni vile vile na hii mambo ya Padri na neema ya Mungu.

Ni kusema neema ya Mungu inatoka kwa Mungu, inapita kwa Padri, kisha inafika kwa Wakristiani pasipo zambi ya Padri kuharibu neema ya Mungu.

3) SIKITIKO KWA AJILI YA LUFU:

Watu wengine wanasema: «Namna gani nitaenda mu Kanisa kwa sababu bibi yangu ao mtoto yangu alikufa? »

Ewe ndugu yangu mpenzi, Kanisa iko na kosa pa hii mambo yako?

Mimi sikwambie juu ya kwenda kufurahi kwa kula ao kunywa pombe na kucheza. Hii utakuwa na haki ya ku kataa.

Lakini apa ninakushauria juu ya kwenda ku nyumba ya Mungu. Ku ile nyumba utakutana na Mwokozi Wako. Utapokea ulinzi wa roho yako. Utasikia ku Evangelio na mahubiri ya kama udugu yako ao mtoto yako hafe, lakini anaishi katika uzima wa milele.

Anaishi fasi moja muzuri zaidi kupita furaha ya hii dunia. Ndani ya Kanisa unaungana katika sala pamoja na ndugu zako walisha kufa. Unajua faida gani atapata ule ndugu yako alisha kufa kama wewe unamuombea katika Liturgia. Kanisa iko moja lakini kipande moja iko apa duniani na kipande ingine iko mbinguni, alafu hii fasi zote mbili mulinzi na Mwokozi ni Bwana Yesu Kristu. Ndani ya Kanisa muombe hivi: Ee Bwana, Mungu wangu pumzisha roho ya huyu ndugu yangu». Halafu huyu mtu atapata faida munene tena wewe utapata ulinzi wa roho yako. Ujuwe ya ndugu yako hakufe, lakini analala na anakuongojea.

4) MAMBO YA KAZI

Ni zoezo mara nyingi wa mama wanatuambia hivi: «Inapashwa kufagia nyumba yangu, kusafisha manguo, ku kona na kupuputa nguo fulani ao bulangeti pa kitanda ao kutayarisha chakula cha watoto».

Lakini, kweli ndugu unaheshimia utukufu wa tumbo unazarau kanisa?

Lakini, dada yangu nani anakuonyesha ya kama usipige chakula na usifagie nyumba yako? Kama unapenda Bwana Yesu Kristo na Kanisa yake na wokovu wako utatayarisha chakula chako mangaribi ya siku ya sita (muposho), kufika asubui ya siku ya Mungu utaenda ku Kanika. Kwa sababu ule mtu anasikia hamu ya kwenda ku Kanisa, hakuna kitu kile kitamuzuia.

Wa Baba wao weko na zoezo ya kutuambia hivi: «Nani anasema ya kama Kanisa haina muzuri? Kweli iko muzuri lakini hii siku ya Mungu ma kazi ni mbalimbali. Kwa mufano: inapashwa kuwandikia ndugu zangu barua fulani, kutengeneza mambo ya kazi yangu, kwenda fasi fulani na kupumuzika ao kwenda kuwaangalia ndugu fulani juu ya kuzungumuza naye.

Ewe ndugu yangu mupenzi, hazienee zile siku sita za juma kwa kufanya hii mambo yako yote? Inapashwa kuharibu na hii siku ya Mungu ?

Inapashwa kujua ya kama hii makuta unapata siku ya Mungu ni moto. Na hii moto itaunguza makuta yako ingine. Wewe tumika siku ile unapenda, lakini Mungu atakupa ile makuta yeye anapenda.

Sabato (dimanche) ni siku ya Mungu ndivyo anavyosema katika Agano la kale: «Siku sita utatumika na kufanya kazi zako zote, lakini siku ya saba utapumuzika na utajitoa kwa Bwana Mungu Wako». Kazi yako ya kwanza ni kwenda ku misa kuomba na kusikia neno la Mungu.

Lakini apana paka wewe peke, lakini lazima tena na wazazi na watoto. Kwa sababu watoto kama hawazoei wakati wangali wadogo hawataweza kuzoea wakati watakua wakubwa. Siku ya saba utagombana juu upate neema ya Mungu rohoni mwako.

Kwa sababu kila mtu eko na mwili na roho. Lakini roho yake ina mafaa mengi kuliko mwili wake.

Ni lazima kutumika siku sita kwa kusaidia roho na siku moja kwa kusaidia mwili yetu. Lakini Mungu alitupatia siku sita juu ya mwili na siku moja tu juu ya roho. Halafu, sisi tutaharibu hii siku moja tu ya roho Mungu alitupatia?

Muhubiri mmoja alihubiri hivi ndani ya Kanisa: «Mutajiri mmoja alikuta masikini mmoja njiani. Huyu masikini alimwonyesha mateso yake. Mutajiri alimuhurumia pa ile makuta saba ya zahabu alikuwa nayo alimupa mbili yule masikini. Wakati kidogo, yule masikini alimuonyesha tena mambo ingine ya sikitiko, yule mutajiri akamupa tena makuta mbili ya zahabu. Wote wa wili wakasafiri kidogo, wakafika karibu ya chemchem na ule mutajiri akamupa chakula yake ule masikini. Huyu akamwonyesha tena mateso yake ingine huyu mtajiri akamupatia makuta ingine mbili.

Makuta yote alimupa ilikuwa sita. Na akachunga likuta moja tu. Kisha kupokea ile makuta sita ule mtu hakupiga aksanti akatosha kisu yake mu mufuko na akajaribu kugombana na yule mutajiri juu ya kumunyanganya ile likuta yake moja ya mwisho. Halafu muhubiri aliuliza kundi la wa kristiani wake: «Ninyi munawaza nini juu ya hii kazi mubaya anafanya huyu masikini? Wa kristiani wakajibu: Auwawe! Muhubiri akawaambia ya kama ninyi munastahili hii malipizi, kwa sababu ninyi munakataa ku mupigia Mungu aksanti. Mungu alitupatia siku sita za kazi ya mwili na anatuomba paka siku hii moja tumuabudu Yeye. Lakini ninyi munanyanganye na hii siku yake moja.

Kweli watu wengine kwa ajili ya kazi yao ya bure, wanaacha Kanisa na hii siku ya Mungu, wanatenda zambi mbalimbali. Watumishi wanatumika na akili muzuri, na uzima safi na sifa mbele ya watu wengine wote siku sita za juma, paka siku ya Bwana.

Wanapoteza makuta yao na kutenda zambi mbalimbali: Kunywa pombe kuiba na kucheza …. kwa hivi, wa kristiani wanakataa kutakasa roho zao, wanatayarisha njia hai ya kwenda mu gehena. Wale watu hawaendake mu Kanisa, hawajue zawadi ngapi za roho wanapoteza; ni vile neno la Mungu linasema juu ya kupenda kukaa inje ya Kanisa. Kwa mufano kila siku ya Mungu Mapadri wanagawanya kwa kila kristiani gramme mia moja ya zababu. Ninyi munawaza nini, wao watakataa kuingia mu Kanisa? Ninawaza wao watafika tangu usiku mbele ya Mapadri kufika!

Halafu, musifanye kazi tena moja siku ya Mungu asubui. Kwa sababu kengele inalia na inatuita kwenda ku misa kufanya sala namna ya tatu: ya kwanza kumushukuru Kristu kwa ajili ya hii siku sita tulitumika. Ya pili kumuomba vile vitu tunataka. Ya tatu kumutukuza.

Katika miaka 1844, Mfalme wa Russie Nikolaos ya kwanza aliendа mu Londres kule inchi ya Ingreza, akaomba aende kuangalia kiwanda (usine) siku ya Mungu (dimanche). Alituma musaidizi wake kumpasha habari ule mukubwa wa chapu. Ule mukubwa akajibu: «Hii chapu hakuna kazi siku ya Mungu asubui». Mfalme akajibu inapashwa kuifungua hata saa mbili.

Na mutakuwa na mapendo yangu na matabishi yangu. Mukubwa wa chapu akajibu: «Ninapokea mapendo yako wewe mfalme lakini, nikiwaambia Watumishi wangu kutumika siku ya Mungu wao watakataa kwa sababu hii amri yangu haipatane na amri ya Mungu. Watumishi wangu wataenda asubui ku Kanisa.

5) <u>RADIOPHONE</u>

Watu wengine wanasema: Wanasililiza Litrugia ku radiophone ao ku magnetophone. Ndugu yangu mpenzi, radiophone ao cassetophone ni ya wagonjwa ao ya wale watu wenye kusafiri njiani ao baharini. Apana ya wale watu weko na afya njema, kwa sababu hawa wanapashwa kwenda ku Kanisa. Ndani ya Kanisa kazi ya kwanza apana ya kusikia wimbo lakini ni sadaka ya Kristo. Hii sadaka ya Komunyo Takatifu haiwezi kufanyika ku nyumba. Ni sawasawa na yule mtu anasikia harufu ya nyama lakini yeye hakule ile nyama.

6) SAFARI

Hii miaka ya mwisho watu wengi wanazoea kuendelesha kusafiri wakati wanasikia kengele ya Kanisa. Na asubui ya siku ya Mungu tunaona vijana wanaume na wanawake. Watoto na wazee wanatafuta motoka ya ku safiri kuenda ile fasi wanapenda. Wao mara ingine wanaweza kutwaambia: «Sisi tunatumika juma muzima, sasa leo tunatafuta kupumuzika, kupata pepo kidogo safi, hakuna mtu yule atatukataza juu ya hii pepo».
Sisi tunawauliza: «Ninyi kweli munapumuzika pasipo sala na baraka ya Mungu mu Kanisa? » Tunaitika ni lazima ninyi kusafiri. Lakini hamuwezi kwenda saa mbili ao tatu mu misa? Ao hamuwezi kutengeneza programme moja juu ya kuingia mu Kanisa moja mu njia? Ni vizuri sana kutayarisha safari yenu paka na mawazo ya kikristu juu ya kufanya sala na kuimba nyimbo njiani munapoenda mukifikiri ninyi wote Kanisa moja.

7) KAZI YA MWINDAJI

Watu wengi hawaingie mu Kanisa asubui. Kwa sababu wanabemba bunduji, mishale, imbwa na vitu vingine vya kuua nayo wa nyama na wanaenda mu pori juu ya kuwinda nyama, ndege na vitu vingine. Wengine wanaenda na makila ku bahari ao ku mutoni juu ya kuvua samaki. Faida ya hii safari ku fasi mbalimbali ni nini?

Sahani ya mvuvi na mwindaji mara kumi iko wazi na mara moja iko ya kujaa. Siku nyingi wanazunguka mu pori juu ya kuwinda nyama na wanarudi ku mulango pasipo hata chakula kidogo. Sisi tunauliza kwa yule mwindaji anaenda mu pori: Wataweza kuacha Kanisa juu ya kwenda kuzunguka bure mu pori sababu ya ndege moja, kalulu moja wa pori, samaki moja? Huyu mwindaji atatujibu hivi: «Kila mtu eko na zoezo yake». Mungu anatuambia hivi: inapashwa kugombana juu ya kuacha zoezo mubaya, fwata Kanisa yake juu ya kusikia mafundisho mazuri na kupata wokovu wa milele.

8) MAMBO YA KULALA

Mtu mwingine anatuambia hivi: «Ewe ndugu yangu ninatumika siku sita kila juma mimi sitaweza kulala usingizi siku ya Mungu? ».
Sisi tunamuuliza: Hauwezi kulala siku ingine? Yeye anajibu: Niko na kazi.

Ndugu mpenzi, siku ya Mungu inapashwa kwenda ku Kanisa. Kwa kazi yako, unaongopa mukubwa wa kazi yako, lakini hauongope Mungu Baba Yako wa roho? Kama hautaenda mu kazi utapoteza makuta yako ya siku. Lakini haupende kuwaza utapoteza nini kama haupende kuingia mu Kanisa? Unasema: «Unapenda kulala siku ya Mungu asubui. Nakujibu hivi: lala siku ya sita (muposho) mangaribi. Acha michezo ya kunywa pombe, ya kwangalia Video siku ya posho, hii yote ni michezo ya shetani. Hii mangaribi inafai kutayarisha roho, ni kusema: Kuungama, maana kutubu zambi zako, na kama uko na baraka ya Padri utaweza kula mwili na kunywa damu ya Bwana Wetu Yesu Kristu siku ya Mungu.

Inapashwa kusoma sala ya komunyo Takatifu. Utasoma Matendo ya Mitume na Evangelion ya kesho. Utafanya sala ya Kristu. Utasema: «Bwana wetu Yesu Kristu Mwana wa Mungu, uniruhumie mimi mwenye zambi». Kisha utazungumuza mambo ya Bwana wetu Yesu Kristu pamoja na watoto wako na ndugu zako. Kisha utapumuzika.

## **S E H E M U  Y A  I N E. -**

Matayarisho ya kwenda ku Misa

1) Matayarisho ya roho.

Kila siku ya Mungu mwaminifu mwema anawaza Kanisa na anaongojea siku ya kwenda ku Kanisa. Mutu mwenye kumpenda kweli Mungu anapenda na Kanisa yake vilevile. Kwani ni kule anapata furaha na amani ya roho yake.

Kama kila siku ya Mungu, unakataa kuwaza faida ya Kanisa, mtu siku ya Mungu asubui hautaweza kuchunga akili yako safi kwa sababu mawazo yako mengi inapenda kuondoa akili yako muzuri inje ya Kanisa. Ni vile na mwili wako, utaingia mu Kanisa lakini akili yako itazunguka mu pepo sababu ya mambo yako mbalimbali.

Siku ya sita (mu posho) kama kwiko namna utanawa mwili yako na kusafisha manguo yako. Kama unatembelea ndugu yako mmoja utavaa nguo safi; mu Kanisa utaenda pasipo nguo safi? Hii kazi utafanya mu Mposho kwa sababu mu siku ya Mungu utaenda asubui kabisa ku Kanisa. Matayarisho ya roho ni namna ya kwangalia hali ya roho yako, ni kusema: hii makosa yako ya zamani juu ya kuomba huruma kwa Mungu. Utawaza sababu ya kumushukuru. Apana kusahau ya kama hii siku ya sita (posho) shetani atakuzuia mingi sababu ya kubaribu mapendo yako ili usipokee neema ya Mungu. Atakukataza usienda mu misa na usipate neema ya Mungu. Zaidi shetani atakugombanisha kama unapenda ku kumunika.

2. - WOGA WA MUNGU.

Waza ya kama unaenda ku Kanisa utasimama mbele ya Mungu. Kama unasimama mbele ya mfalme mmoja ao Patriarche utasimama na heshima mingi. Halafu mbele ya Mungu utasimama na kufunga mikono yako ku mukongo? Ao utasimama pasipo haya? Mungu eko katikati yetu pasipo sisi kumuona, ni vile yeye anataka na anasema hivi: «Hakuna mtu hata mmoja ataweza kuona sura yangu na ataishi».

Kwa sababu nani ataweza kusimama mbele yake? Kama Nabii Isaya alivyoagua: Mungu eko yulu pa kiti chake Malaika wengi wanamuzunguka pembeni yake na wanamutukuza. Wewe unashangaa na anapaza sauti na kusema: «Mimi ni mutu mwenye zambi? »

Sisi tutasema nini? «Wana wa Israeli wakati waliona mulima wa Sinai inatosha shimoko na waliposikia baragumu, wakaogopa kuijongea kwa sababu Mungu alipenda kushuka na kuzungumuza na Nabii Musa.

Na huyu Musa wakati alishuka toka Mlima Sinai, wao hawakuona uso wake kwa sababu iliangaa na nuru kimungu. Sisi namna gani tutasimama ndani ya Kanisa kama tunaona tunakula na tunakunywa mwili na damu yake? Pasopo mingi na woga mbele ya Bwana wetu Yesu Kristu. Hii mapendo na woga ndani Kanisa inauwa hii zoezo mbaya.

Kabisa kabisa Watumishi wa Kanisa, ni kusema Padri, Shemasi na Waimbaji wanazoea hii kazi ya Kanisa hawamuogopa Mungu. Ku mwanzo wanaogopa lakini wakati wanaingia ndani ya Kanisa pole-pole hii woga inaisha na wanazoea mbaya sawa wanaingia ndani ya nyumba yao ao ndani ya soko. Ee ndugu yangu, wakati unaingia ndani ya Kanisa ikaa pa kiti chako, simama, fanya sala na usizungushe macho yako ndani ya Kanisa yote kwa kwangalia nani anaingia na anavaa nini. Usiwaze kazi na mambo yako, hii yote acha inje ya Kanisa.

Tunaimba hivi katika wimbo Hieroviko: «Kila wazo la uzima wetu tunalitosha inje». Wengine wanaenda ku Kanisa lakini akili yao wanawaza kazi yao. Wakati fulani kulikuwa ndugu wa wili wavuvi. Mmoja aliwaambia ndugu yake: «Mimi ninaenda kila siku ya Mungu ku Kanisa lakini wewe unakaa hapa». Kweli yeye anakaa ku kazi yake, lakini akili yake ilikuwa ndani ya Kanisa.

Anatumika na mtumbwi yake na anawaza wanasema nini na wanaimba nini ndani ya Kanisa. Na yeye ananza kuimba ndani ya mtumbwi yake: «Uliye watamani …. kila Mwenye mpumzi ……DOXOLOGIA na anaendelesha wimbo wa Liturgia». Hivi yeye na akili yake anafwata mustari ya sala ndani ya Kanisa, ule ndugu yake alienda mu Kanisa, na akili yake anangalia kazi gani anafanya ndugu yake katika maji anavua samaki, anaingiza wavu ndani ya maji? Sasa nauliza nani anapata faida ya roho kupita mwingine?

3) PASIPO MAZUNGUMUZO

Ule mtu anazungumuza ndani ya Kanisa hawezi kufanya sala. Anazuia ndugu yake kuomba. Mambo yote ya nyumba na ya kazi inafai kuizungumuzia inje ya Kanisa. Tuko na wakati mingi ya kuweza kutengeneza mambo yetu inje ya Kanisa. Wengine wanashimanga ndugu zao ndani ya Kanisa juu ya ile mavazi yao wanavaa. Kuna amri ya Bwana Yesu Kristu ya kwacha kushimangana. Kila mkristiani ndani ya Kanisa inapashwa kunyanyua roho yake kwa kuzungumuza na Yesu Kristo, kumwambia mambo na sikitiko yake juu ya kupata saidio ya roho. Tena ni mubaya kucheka ao ku geuza fasi ya kukaa, na kuleta makelele ndani ya Kanisa. Wengine wanafananisha pole-pole sauti ya Mapadri ao ya Waimbaji pasipo kuwaza ya kama ndugu zao weko na omba na itawasikitisha. Inafaa kuwa na utazatibu na kukaa kimya ndani ya Kanisa. Waimbaji na Mapadri wanaimba juu ya kusaidia waaminifu wengine kuomba ndani ya roho yao. Kama Padri analeta ruhusa kuiko namna ya kuimba pamoja nao.

4) WAKATI GANI INAPASHWA KUKAA AO KUAMKA NDANI YA KANISA. -

Kama ndani ya Kanisa muko viti kuna namna ya kukaa, lakini apana wakati wote. Inapashwa kusimama wakati tunasoma Zaburi ya sita (Eksapsalme), Uliye watamani, Evangelio ya asubui, Doksologia ukubwa, mwanzo wa Liturgia Takatifu na wakati Padri atatoka na Evangelio ku mikono yake, wakati atasoma Evangelio; wakati waimbaji wataimba wimbo wa Hieroviko, wakati wa Symvolo ya imani; ni wajibu kweli, Baba yetu na ile wakati Padri ataleta Komunyo Takatifu kwa wakristiani, na mpaka mwisho wa Liturgia. Wakati Padri anapazaa sauti na kusema: «Vilivyo vyote vinatoka kwako», sisi wote tutapiga magoti kwa sababu ile wakati roho Mtakatifu anashuka pa meza Takatifu na anafanya fumbo (mystere) ya kugeuza mukate na vinyo kuwa mwili na damu ya Bwana Yesu Kristu. Hii wakati ni wakati wa mafaa wa Liturgia Takatifu. Ndani ya Kanisa inafaa kuacha viti wazi juu ya wagonjwa na wazee. Kama tunaona wa mama, wazee, na wagonjwa wanaingia ndani ya Kanisa, ni lazima sisi kuwachia fasi yetu.

5) ALAMA YA MSALABA. -

Msalaba ni alama ya ushindi juu ya lufu na shetani. Bwana Yesu Kristu alimwanga Damu yake juu ya Msalaba analeta wokovu na utakaso kwa wale watu wanamwamini. Ni hivi, kama tunafanya sala mu nvumba yetu ao ndani ya Kanisa inapashwa kufanya alama ya Msalaba. Mapadri na walimu ya waminifu wetu (Catechistes) wanapashwa kutufundisha alama ya Msalaba ya kweli. Tunafanya hii alama ya Msalaba kama tunaanza sala fulani, kama tunasikia jina la Utatu Mtakatifu, jina la Mtakatifu wa ile siku, jina la Yesu Kristu na Mzazi-Mungu na wakati tunasikia Sinaksari ya Watakatifu (Ma jina ya Watakatifu ya kila siku asubui), kama tunabusu Icone na Evangelio ao tunapokea Komunyo Takatifu. Kama tunaenda kupokea baraka ya Padri ao Antidoro. Hatufanye alama ya Msalaba, wakati Padri anatufukizia na chetezo, tutainamisha paka kichwa yetu.

6) MATAYARISHO YA KUPOKEA KOMUNYO TAKATIFU

Kazi ya wa Catechistes ni ya kuweka vizuri wa Kristiani mu mistari wakati wanakuja kupokea Komunyo Takatifu. Haina heshima mwaminifu kusukuma mwenzake ndani ya mustari. Kwa sababu sisi wote mbele ya Mungu tuko mu umoja. Sawa vile

waaskari wanapita mbele ya Mfalme wao, na sisi vilevile tutaweza kupokea ufalme wa mbinguni.

Ndani ya roho yetu inafai kusema neno la Munyangani: «Ee Bwana, unikumbuke mimi katika ufalme wako». Apana kuwa na chuki ndani ya roho juu fulani. Si Vizuri wakati unaenda kupokea mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristu utoshe ulimi yako inje. Kisha kupokea Komunyo Takatifu, utapanguza midomo yako na hii nguo nyekundu. Kama wengine wanafanya kosa, wewe ndugu yangu, apana kusirika. Kama unapenda utaweza kuwashauria inje ya Kanisa, kama Padri wa membres wa Comite ao Catechiste wanakufokea kidogo juu ya mambo fulani, wewe pokea neno lao; hii neno leo litakusaidia wewe. Ya kwanza ni wanaume watakomunika wa kubwa na watoto; kisha wanawake wakubwa na watoto. Kama ndani ya Kanisa muko Mabikira (Soeurs), watawa ao wagonjwa ni wao watakomunika mbele.

Hii siku ya Komunyo Takatifu, tutafanya nguvu juu ya kwacha kutema mate.

Si lazima kisha kukomunika wewe kubusu tena Icone kwa sababu unapokea Mwokozi muzima katika mwili wako. Mbele ya kukomunika kwiko namna ya kubusu Ikone ya Watakatifu juu ya kuomba saidio yao.

7) <u>MWISHO WA LITURGIA. -</u>

Watu wengi sisi tunawaona, wanacheka, wanasalimiana karibu ku mwisho ya Liturgia ao Mafumbo ingine, wanajibusu na wanaleta makelele. Hii mambo yote ni ya kufanya wakati misa inaisha na sisi tunaenda inje ya Kanisa. Ndani ya Kanisa inafaa kukaa sawa Malaika wanazunguka kiti cha ufalme. Na mapendo yetu tutaionyesha kwa ndugu zetu inje ya Kanisa. Ni lazima kwa wakristiani wote kuonana inje na kuzungumuza mambo yao ya furaha, kusalimiana na kutayarisha mapatano yao ya siku ingine. Kanisa si nyumba ya wageni, pahali kila mtu anaingia, anakula na anatoka. Ni nyumba ya Mungu Baba Yetu, na inatupatia wakati muzuri juu ya kupatana mmoja kwa mwingine fasi moja kwa kuzungumuza mambo ya roho sawa watoto wa Baba moja na ndugu katika roho.

8) <u>MATAYARISHO YA KUBUSU IKONE</u>

Kanisa yetu tangu wakati ya Bwana Yesu Kristu inachunga Ikone ndani ya Kanisa. Historia ya Ekklezia yetu inatuambia ya kama Mwevangelisti Luka alikuwa mtungaji wa Ikone ya Mzazi-Mungu. Alipeleka hii Ikone kwa mama Maria na yeye aliibariki na akasema hivi: «Hii neema inatoka kwa Mwana wangu Yesu Kristu na baraka yangu natakia Ikona ikae milele».

Mtakatifu Vasilios Mkubwa anatufundisha ya kama ikone ni sawa kitabu cha wakristiani kama tunaona Ikone moja tunakumbuka uzima ya huyu Mtakatifu, mateso alipata yeye kwa ajili ya imani kwa Kristu na tunapenda kubusu na kusifu uso Wake.

Hii sifa na heshima haiende ku lumbao ao ku rangi lakini inaenda ku sura ya huyu Mtakatifu. Watakatifu ni ndugu zetu, wa kubwa na marafiki ya roho zetu. Wao wanasikiliza maombi yetu na wanapeleka mambo yetu kwa Mungu.

Tunaweza kuomba kwa Mungu lakini na Watakatifu wanasikia maombi yetu na wanatusaidia. Watu wa makanisa ingine wanatustaki, wanasema sisi tunabusu sanamu. Ni uwongo kwa sababu Ikona si sanamu. Ya pili, tunamwabudu Mungu na tunabusu Ikone. Kama mtu mmoja anaingia ndani ya Kanisa, ya kwanza atafanya alama ya Msalaba, na kisha atabusu Ikone iliyo ku mlango ya kanisa: Mwisho ya Liturgia kama unapenda kuiko namna ya kubusu ikone ya Ikonastase (mbele ya Ieron). Mu nyumba yetu kwiko namna ya kubusu ikone ya Watakatifu kila wakati tukiwa na matakio na mapendo.

## S E H E M U   Y A   T A N O

## KAZI YA KANISA SI YA BURE

Watu wengi wanasema ya kama hii mustari na zoezo ya sala haina na faida ya roho. Lakini neno lao ni uwongo kabisa.

1) LITURGIA KIMUNGU. -

Ya kwanza hii Liturgia iko katikati ya ibada yote ya Kanisa. Pasipo hii hatuwezi kupata ufalme wa Mungu. Kanisa iko sawa nyumba ya mwisho, na kutoka hii nyumba tutaenda mbinguni. Munajuwa juu ya nini? Kwa sababu ndani ya hii Kanisa munafanyika sadaka, ni kusema Yesu Kristu anajitoa: Mwana-kondoo wa Mungu. Hii inatupatia kila wakati chakula cha roho, mwili na damu yake. Anatupatia uzima wa milele, yeye mwenyewe anasema: «Kama mtu anakula hii mkate (mwili wangu) ataishi milele». Vitu vyote vizuri vinatoka ku hii sadaka.

Mbele ya kufika Yesu Kristu mu hii dunia, watu wote waliharibu uzima na tabia yao kwa Mungu kwa ajili ya zambi zao zote. Wote walisikitika juu ya hii zambi na walipenda ku mufurahia Mungu; lakini namna gani wataweza kufanya vile? Walichinja wanyama yao, na hii nyama, walitoa sadaka kwa Mungu juu ya kupata huruma yake wakati watapakaa damu ku mwili yao.

Lakini walisamehewa? Apana. Walisikia paka makosa ya zambi zao. Ilifai kumutolea Mungu kiumbe moja chenye kupita wa nyama juu ya kumufuraisha Mungu. Na ile sadaka yenye kumupendeza Mungu alikuwa Bwana Yesu Kristu. Huyu alibeba zambi za watu wote pa mabeka yake juu ya kuwaokoa. Mungu baba yake alipokea sadaka yake kwa sababu ni sadaka ya mapendo mingi. Mungu ni mapendo, kwa hivi alimupokea na anamupenda kila mtu. Tangu ile wakati iliisha sadaka ya wanyama.

Kisha sadaka yake Yesu Kristu Msalabani, Kanisa yetu iliweka hii sadaka kwa kila Liturgia.

Na tena Bwana Yesu Kristu alitoa mwili wake juu ya sisi kuokolewa. Hakumwanga Damu yake mara ya pili. Roho anashuka pa Meza Takatifu, na hii vitu Vitakatifu tunamutolea, ni kusema mkate na vinyo anavigeuza kuwa Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristu. Hii inafanyika kwa fumbo kweli ya ajabu. Kila mara Mungu anapokea hii sadaka ya Mwana Wake mpendwa, na anahurumia zambi zetu sisi katika hii sadaka tunapokea kweli Bwana Yesu Kristu muzima.

2) PROSFORO

Maana ya hii jina «Prosforo» ni kusema: Minatoa, minaleta zawadi kwa Mungu. Mungu haombe kwa sisi zahabu ao vitu vya bei mingi kwa sababu yeye anajua sisi hatutaweza ku mutolea hivi vitu. Alipata namna ingine moja ya wepesi, ni mkate na vinyo, na yeye ataturudishia Mwili na Damu Yake kwa sababu inafanyika miujiza. Unawaza ndugu yangu, sifa gani mukubwa uko nayo kwa Mungu kama unatoa moja Prosforo, juu ya kufanya Mwili na Damu ya Bwana Wetu Yesu Kristu? Ni desturi ya zamani kwa waaminifu wetu juu ya kusopoka sana wakati wa matengenezo ya hii Prosforo. Ule mwanamuke alipenda kufanya Prosforo anapashwa kuishi mu ubikira ao akuwe msiyeolewa (bibi wasipo bwana). Mbele atavaa manguo safi kiisha atafanya sala, na hivi atafanya kazi ya kutengeneza Prosforo. Kama matayarisho yetu iko ya kweli na Mungu atatupatia neema mingi.

Watu wengi hawasadiki ya kama mkate na vinyo hii tunaona ni Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristu. Lakini sisi hatuwezi kweli kula damu na nyama muzima. Mungu alipata hii namna sisi tunaona kweli mkate na vinyo lakini tunapokea Mwili na Damu yake ya kweli. Ni vile anafanya Mungu ku mambo ya maziwa ya mtoto mchanga. Maziwa ni

nini? Ni damu. Inatoka ya roho ya mama yake, inaenda mu kilari na inageuka inakuwa maziwa mweupe. Juu ya nini? Kwani mtoto hawezi kunywa damu. Kama anazoea kunywa damu wakati atakomea atazoea kuuwa watu juu ya kunywa damu yao. Ku mukongo ya hii maziwa tunaona damu ya mama yake. Na ku mukongo ya hii mkate na vinyo tunaona mwili na damu ya Bwana Yesu Kristu.

3) MAKUMBUSHO YA WAAMINIFU

Tulisema ya kama mu kila Liturgia mu nafanyika sadaka ya Yesu Kristu. Ni desturi mu Kanisa Orthodoksi waaminifu, kwa kila Liturgia, Kupeleka kartasi (papier) pale peko majina ya wandugu zao wazima na wafu. Ni juu ya nini? Kwa sababu kwa hii saa ya matayarisho ya fumbo ya Komunyo Takatifu Padri anatosha makombo (sehemu) ya Prosforo kwa sifa na makumbusho ya Mzazi-Mungu, ya majeshi ya Malaika na ya Watakatifu Wetu wote. Kisha anatosha sehemu ya Prosforo kwa ku kumbuka na jina ya wafu. Wale watu wote Padri alianza kukumbuka wanaungana katika kikombe Takatifu pamoja na Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristu. Mungu anawapumzisha wale walikufa lakini na wale wazima anawape ulinzi na baraka kwa mufano: «Mkubwa mmoja wa Monasteri jina lake Padri JACOBOS alikufa mu 1992 siku moja ya Mungu asubui alifanya matayarisho ku Prosomidi. Katikati ya majina ingine alikumbuka jina la mtu mmoja Agapios, mara moja akasikia sauti yake ilimwambia hivi: Na kushukuru, ewe Padri wangu kwani unanikumbuka katika hii sala. Padri alimujibu: «Mtoto yangu uko wapi? Yeye akasema: Niko ndani ya nyumba moja ya giza sana na ninateswa sana. Wakati wewe unanikumbuka ku Proskomidi mwangaza inakuja inasambaza hii giza wakati kidogo na ninasikia furaha kidogo». Mufano ingine, katika mwaka 1922 kulikuwa vitu katikati ya inchi ya Creece na Turque, jamaa mojaa ilituma mtoto yake ku hii vita. Lakini wazazi walimufanya sala mtoto yao. Siku moja asubui saa ya 5 h 00’, ile wakati wazazi yake walifania Liturgia, mtoto yao ule askari alifanya nguvu na alitoka ku mikono ya maadui; yeye alipata uzima wake sababu wazazi wake walimufanyia Liturgia.

4) MISHUMAA (BOUGIES)

Sisi waorthodoksi tuko na zoezo ya kuwakisha mishumaa (bougies)kwa kila sala. Sababu gani?

1) Ya kwanza juu ya kuleta mwangaza;
2) Ya pili tunapenda kutoa zawadi kwa Mungu. Maana ya mfano: «Vile Mushumaa inaregea wakati tunaiwakisha na inaisha; ni vile anapashwa kuishi kila mwaminifu mu uzima wake. Ni kusema kwangaza fazila yake na kuregea katika mapendo ya Mungu. Mtakatifu Athanasios, Patriarche wa Alexandria anasema: «Sisi tunatolea mishumaa, ubani na Mafuta. Hii yote Mungu anaipokea kwa sababu ni sawa masikilizano na Mungu Wetu.
3) UBANI

Na kazi ya ubani ni mbili:

Tunatolea ubani kwa Mungu sawa pepo ya harufu ya roho juu ya kututumia sisi neema ya roho Mtakatifu.

Ya pili tunatolea ubani juu ya kufukuza shetani, yeye kama anasikia harufu ya ubani anakimbia kwani hataweza kuvumilia. Ndio vile tunafukuza ile wakati ya Doxologia kwa maana itaanza Liturgia kimungu juu ya kutoka pepo mchafu ndani ya Kanisa. Kwa hivi tunafukuza ubani ku mwanzo ya ubatizo juu ya kutosha kila shetani wa giza mu maji.

Ubani inafaa kwa kila sala ya Kanisa.

## SAUTI YA MWISHO

Unaona, ewe Msomaji wangu, faida gani tunapata kama tunaenda ku Kanisa. Tunapata fazila ya roho na tunapumuzika katika Roho na Mwili. Tunapokea nguvu ya kushindana na mateso na majaribu mu uzima wetu.

Baraka mingi ya Mungu inakuja na tuko na furaha na amani. Lakini vitu ngapi Takatifu tunapoteza kama tunaikaa inje ya Kanisa? Ndugu yangu, usikae bure. Kamata mupango tangu leo juu ya kwenda ku Kanisa ili upate kwendelea. Acha mambo yako ya kukataa, wende ku Kanisa. Kazi hata moja haiwezi kukuzuia, paka magonjwa ya nguvu. Padri mmoja wa roho alisema ya kama hawende ku Kanisa nyumba yako yote itaungua. Wewe utakaa mgonjwa ndani ya nyumba yako. Musisahau ya kama pasipo kwenda ku Kanisa juma tatu, Kanisa itakupatia malipilizi. Ni vile inatwambia kanuni moja ya Baraza Ikumeniki ya Sita. Inafai kwenda kila mara ku Kanisa, chukua ndugu zako wote na jamaa yako.

Zaidi chukua pamoja nawe wale watu wamakuisha kutoka ku Kanisa, na utawasadia juu ya roho yako iungane na Kristu. Hivi wao vilevile waokolewe kwa sababu inje ya Kanisa hakuna wokovu, ni vile wanasema Watakatifu wetu. Mungu atakulipa malipo ya roho kama Wewe utaweza kushauria na kupeleka mtu mmoja ku Kanisa. Kama hauwezi kumusaidia na neno la upole umupe hii kitabu.

Natumainia Mungu atamusaidia, atapenda kufwata hii Kanisa, hivi utamutukuzwa Bwana Yesu Kristu sawa mtoto yake wa kweli, na utaishi na kitumaini ya kupata wokovu wako juu mbinguni.

Usinisahau na mimi niliandika hii kitabu. Sipokee makuta. Kitu ninapenda juu yako wakati unaingia mu Kanisa unikumbuke kwa kuniombea, hata mimi ni hai wala nimekwisha kufa.

# KITABU YA MBILI

## JUU YA NINI UNAKATAA KUUNGAMA

Mbele ya kwenda kwa Padri wa roho, inafaa Wewe peke kuangalia na kufahamia ndani ya roho yako. Nikusema Wewe peke unapashwa kutazamia kabisa ndani ya roho yako. Inafaa kuangalia hali ya mwili wako. Kuangalia wakati gani na mara ngapi ulivunja sheria Takatifu, ulitenda zambi kwa matendo mabaya.

Sasa anza wewe mwenyewe kuangalia na utaratibu mingi ya kwanza:

I. ULIMI YAKO.

Zambi mingi inatoke wakati ku ulimi yetu. Kwa ajili ya ulimi yetu. Kwa ajili ya ulimi yetu inakuja Wakati ingine lufu ndani ya roho yetu ao wakati ingine uzima wa milele. Nabii na Mfalme Salomon anatuambia:
«Ni nani hakutenda zambi na ulimi yake ? . Ni kusema watu wote wanatenda zambi kwa ulimi wao. Hii zambi ni mbalimbali.

1. - ZAMBI YA UWANGO. -

Ulimi ya watu inasema uwongo kila siku. Lakini, kila neno ya uwongo si zambi kidogo. Watu wengi wanatuuliza: Ewe ndugu yangu kama ninasema neno moja ya uwongo, hii ni zambi kubwa?
Ewe ndugu yangu mpendwa hakuna tafauti kati ya zambi ndogo na zambi kubwa, kwa sababu mukubwa wa kila zambi ni shetani, adui ya wokovu wetu.

Mungu wetu analipiza kila neno ya uwongo wetu, kwa sababu tunavunja amri yake ya tisa (Amri kumi ya Agano Le Kale). Kwa mfano, ndani ya Agano Jipya tunasoma mu kitabu cha Matendo ya Mitume 5 «ya kama Mtakatifu Mtume Petro aliuwa Anania na Safira. Wale watu walikuwa na shamba moja na kisha waliiuzisha. Hii makuta walipokee wakaileta kwa Mutume Petro, juu ya kukabulia masikini. Lakini walichuga nusu moja ya hii makute yao. Waliweza kuchunga makute yao yote, kwa sababu hata mtu mmoja fulani hawezi kuwaambia walete makuta yao kwa Mtume Petro. Lakini wakati waliitikia kusema uwongo, ya kama watatoa kwa Mutume Petro makuta yao yote juu ya kupata utukufu ya dunia na wasijuwe na watu wengine. Lakini Mtume Petro aliyekuwa na mwangaza kwa akili yake alimuuliza:
«Ewe Anania, juu ya ninyi shetani aliingia ndani ya roho yako, na sana unaniambia uwongo? Haukuseme uwongo kwa watu, lakini kwa Mungu». Palepale ule mtu Ananias alianguka chini na alikufa.
Mungu alimulipiza mara moja. Kisha saa tatu bibi yake Safira alifika pasipo kujua lufu ya bwana yake. Wakati Petro alimuuliza ule Mama alisema uwongo, ya kwamba makuta yote waliuzisha shamba yao walimupa yeye. Halafu na ule Mama alikufa mara moja palepale.

Historia hii ni ya kweli, na Mungu hapa alilipiza wale watu juu ya sisi kujua ya kama Mungu hapendi kusikia neno letu la uwongo. Kabisa kabisa itakuwa malipizi mkubwa ku uzima wa milele, kwa wale watu wenye kusema uwongo na wanakataa kutubu.

2. ZAMBI YA KUTUKANA NA KUHUKUMU. -

Ewa ndugu yangu, uwaze tena ya kama ulisimangana ao ulisema neno mbaya juu ya watu wengine. Kama ulifanya hii tendo inapashwa kujua ya kama uliharibisha sifa ya ndugu zako, uliwahuzunisha rohoni mwao.

Bwana Yesu Kristu anatuambia: Musisukume kusudi Mungu asiwasukume ninyi. Pasopo tena, kama ulimi wa kinywa chako ilihukumu watu watakatifu, ni kusema watumishi ya Mungu, hii zambi ni kubwa kupita. Kila Padri ni Mtumishi wa Mungu na huyu ataleta jibu kwa Mungu. Sisi hatujue kama roho yake iko safi ao iko mbaya. Yeye anatuombea kwa Mungu ili sisi tupate wokovu wetu. Kama Mutu mmoja atachambula Ambassadeur mmoja wa inchi fulani ya ugeni, inchi yake itapata mambo, italipiza ule mtu alisema neno mbaya. Vilevile na sisi kama tunahukumu ao tunachambula Mapadri wetu tutapata mambo munene kwa Mungu wetu.

Sikilizeni historia ingine moja, inatoka mu Agano La kale. Dada ya Nabii Musa yeye pia alikua Nabii Mwanamuke. Siku moja aliuliza hivi: «Mungu alihubiri paka Nabii Musa na hapana ye mimi? Halafu Mungu alimulipiza kwa ajili ya Majivuno yake. Alimupatia magonjwa ya ukoma. Na ukoma yake ilikuwa sawa teluji. Hii zambi iko teke-teke leo. Watu wengi wanawatukana leo watumishi wa Mungu, na kabisa kabisa wale wanafata makanisa ya uwongo wanasema maneno mabaye kwa wapadri yetu juu ya kuharibu imani na roho ya wakristiani yetu na yao. Mtakatifu Konstantinos Mfalme mkubwa alituonyesha hivi: «Nikiona na macho yangu Padri mmoja kufanya zambi moja nitamuzibia na manguo yangu ya ufalme».

## 3. ZAMBI YA MATUSI. -

Matusi ni zambi ya ulimi yetu. Hii kosa iko matata kwa sababu hata shetani hapenda hii zambi. Agano Jinya inatuambia ya kama na: «Washetani wanasadiki na kuogopa, kama wanasikia jina kubwa la Mungu» (Marko).

Lakini wanakataa kumuchambula Mungu. Tuko na mifano mingi ya hii zambi, Mungu analipiza wale watu wenyi kutukana. Angalisho moja: Katika tarehe 27 desemba 1940 waaskari greki waligombana vita juu ya waaskari ya Italia. Siku moja kundi moja ya waaskari greki walipeleka na motokari yao chakula na vitu mbalimbali ku hii vita, mu njia waliona askari moja mwenye kuumiwa. Walimushauria hivi: «ndugu yetu vumilia na tutarudi kwa haraka tutakubeba. Huyu askari mwenyi kuumiwa alichambula Mzazi-Mungu Maria. Waaskari wengine waliogopa wakati walisikia hii matusi yake, kwa sababu ilikataziwa kwa askari yoyote kuchambulana.

Hivi walimwambia: Ewe ndugu yetu, usichambule jina la Mzazi-Mungu. Sema paka: «Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu Maria unisaidie». Lakini yeye hakupenda kusikia aliendelea kuchambulana.

Kisha wakati kidogo alirudia, walimupata amekwisha kufa. Walisikitika mingi rohoni mwao kwa sababu ule askari alitoka mu hii uzima na hii namna. Kwa kuwa hakukukuwe Padri ku ile kundi ya askari, walichimba kaburi na kisu yao na walimuzika. Walifanya msalaba yao na waliendelea njia yao. Wakati walitembea mbali metre makumi mbili bombe moja iliangukia pa ile kaburi, ilipasuka na ilimutosha ule askari na ikamutupa mbali karibu metre kumi. Waaskari wote walianguka chini kwa kulinda miili yao. Kisha walienda karibu walimuweka mara ingine ndani ya kaburi yake na waliendelea na safari yao. Lakini kisha saa kidogo bombe ingine iliangukia mara ya pili pa kaburi ileile, ilimutupa mbali metre kumi. Halafu walisikia ya kama hata udongo ya inchi inakataa ule mtu mwenye ku chambulana. Ni kusema na inchi haipendi kuchunga ndani yake ule askari mwenye matusi. Walimwacha paka vile, pasipo kumuzika, walienda safari yao. Hii mambo iliwaogopesha wa askari. Walitetemeka kwa sababu waliona nguvu na uwazo wa Mungu.

## 4. - ZAMBI YA NENO YA USHARATI. -

Ewa ndugu yangu, inapashwa tena kuangalia kama ulimi yako inasema maneno mbalimbali ya usharati, ao inaimba wimbo ya usharati, ao mazungumuzo ya bure na michezo ya usharati. Halafu hivi ulimi yako iko sawa hii fasi ya uchafu. Biblia Takatifu na

kinywa cha Mungu inatuambia hivi: «kila neno la usharati na uchafu linapashwa kuondolewa kinywani mwenu».
Na kweli, kwani, ewe Mwaminifu wangu, namna gani utaweka Bwana Yesu Kristu, ni kusema mwili na damu yake, ndani ya kinywa chako, humo munatoka uchafu na iko sawa kinywa cha shetani?

## 5. ZAMBI YA KUKATAA DINI YA MUNGU.

Tena inapashwa wewe kuangalia kama unachunga vizuri imani ya Mungu na kama ulimi yako ilitukana imani yetu ao ulikataa imani na Kanisa Orthodoksi.

Hii mambo ya kukataa inafanyika na maneno yako, na matendo yako ao na mufano yako. Juu ya hii mambo inafaa ku kuangalia kama ulizungumuza neno fulani juu ya imani Orthodoksi, ao mbele ya watu wengi ao mu radio ao kwa siri ao waziwazi.

Tena angalia roho yako kama uliandika barua ao kitabu, ao mafundisho ya uwaogo na kama hii fundisho yako watu wengine waliisoma iliharibu imani yao na mufano yao. Pasopo, kama mtu mmoja anafanya hii kazi, anapika mwili wa Yesu Kristu, kwani mwili wake ni kanisa yake.

Tena utangalia roho yako, kama ulienda kusikiliza mafundisho ya ma kanisa ingine ya uwongo, kwa mufano kundi ya Temoin de Jehovah, Kundi ya Kanisa Katholika, wa Protestants, kundi ya Masonia na ingine. Kama ulifanya sala na maombi pamoja nao ulifanya kosa. Hii ni zambi kubwa. Makundi Takatifu ya Makutano ya Ikumeniki inakataza sisi kufanya sala pamoja na watu wa heretiques. Kanisa inaliniza na mafingo wale watu (Mapadri ao Walaiki). Watafanya hii maombi pamoja na wa heretiques.

Mtakatifu Mwevangelisti Yoano, Mwanafunzi wa mapendo anatukataza sisi kupokea mtu heretiques ndani ya nyumba yetu, tena na kama tutamusalimia. Vile anasema katika barua yake ya pili (2 Yoane 10).

Tena inafaa kuwaza, kama ulikataa imani ya Orthodoksi kwa matendo yako, ao kama uliiba vitu vya ma kanisa ya Mungu, ao kama ulipasua ma Ikone ya Watakatifu, ao uliichoma, ao ulizuia watoto wako ao watu wengine kwenda mu Kanisa.
Ao kama ulisoma vitabu vya heretiques na uliipatia watu wengine kuisoma.

Angalia tena roho yako kama ulijitoa ku imani ya Orthodoksi na mufano yako, ni kusema ulikataa kuhakikisha imani yako kwa watu wengine ao unakataa kusema juu ya mafundisho ya kanisa Orthodoksi, ile wakati watu wengine walichambula imani na Kanisa Orthodoksi.
Kumbuka muzuri hii sauti(neno) alituambia Bwana Yesu Kristu: «Basi kila mtu anayekikiri mbele taa watu, nitamukikiri vilevile mbele ta Baba yangu aliye mbinguni. Lakini kila mutu atakayenikana mbele ya watu, nitamukana vile vile mbele ya Baba yangu aliye mbinguni» (Matayo 10, 32-33).

Hii zambi ya kukataa dini yetu ni kubwa sana. Zamani ile wakati Kanisa yetu ilizulumiwa na Wafalme wa Roma watu wengi walikufa lakini wengine walikataa imani ya Orthodoksi kwa mfano nitandika hapa historia ya Mtakatifu shahidi Yakobo wa Persia:
«Huyu kijana aliishi karibu ya mwaka 400 kisha kuzaliwa Kwake Yesu Kristu. Alikuwa mkubwa na rafiki ya Mfalme wa inchi ya Persia. Siku moja yeye aliacha imani yake ya Orthodoksi.
Hii tendo lake lilileta sikitiko mingi kwa Mama yake na kwa bibi yake. Walimuonyesha hivi: Hatupendi kujua hata kidogo juu ya uzima na hali yako. Hauko tena mutoto yangu na Bwana ya bibi yako. Tangu ile wakati yeye alisikia hii sauti ya jambo yake, alitubu, alilia sana na alikamata mipango ya kutengeneza kosa yake. Kwa hii mambo alifika kwa Mfalme. Rafiki yake na alimuonyesha ya kama, alikosa kwa sababu, aliacha imani yake. Mfalme jina lake Izdigerdis, alishangaa. Alimushauria mingi juu ya kugeuza mwanzo yake lakini hakuwezi.

Yakobo alisimama imara ku imani yake. Tena alimuambie: «Ninyi mufanye hii kazi munataka. Mimi nitakufa paka mkristu Orthodoksi. Halafu waaskari wakamuteswa sana

na mateso mingi. Walianza kukata kipande moja-moja ya mwili wote. Ni kusema walikata mikono yake, miguu pasipo kuweza kuharibu mufano na imani yake. Ku mwisho walikata kichwa chake na vile yule kijana Yakobo alikufa shahidi, ndiye Mtakatifu Yakobo».

Unaona, ndugu yangu, ulimi wetu unaweza kutenda zambi ngapi?

## II. - 2. MIKONO YAKO.

### 1. - Kiapo.

Sasa inafaa kuangalia mikono yako, kama uliweka mikono yako yulu ya Evangelia ya Yesu Kristu na ulilapa kwa uwongo mambo moja. Kiapo ni zambi kubwa, wakati mtu mmoja anaapa kusema kweli lakini yeye anasema uwongo. Tena utauliza roho yako kama unatumika kweli ao uko muzaifu.

Ni kusema unapokea malipo yako kila mwezi, pasipo kutumika katika woka ya Mungu na Mapendo ya kazi yako. Kama unataka kusaidia ndugu moja ao jirani yako utamusaidia na makuta ao mali yako na hapana na vitu vya watu wengine. Kama utasaidia ndugu zako na unakataa kusaidia watu wengine wa masikini, vilema na vipofu, hii tendo tako ni mbaya kwa Mungu pasopo, hapana kuiba makuta ao vitu fulani vya inchi yako. Mungu atakuhukumu vikali na utasema nini kwake?

Lakini juu ye nini Mungu anakuja katikati ya hii mambo ya kuapa?

Kwa sababu Mungu ni Mwenyezi tena Mwangalifu kwa vitu vyote vya dunia. Na wewe uliweka sawa Mushuhuda wako ule Mungu wa pekee.

Ni kusema ulimwambia Mungu: Ewe Mungu wangu naape kwako na kwa wale wetu weko uku ya kama nitatumikie kweli inchi yangu na sifa na mapendo. Kisha wewe ulivunja ahadi yako kwa Mungu na uliharibu Mapendo ya Mungu. Hii kosa yako iko nguvu sana na wakati moja Mungu atakulipiza.

Tena watu wengi, kama weko na mambo wanaenda ku nyumba ya kuhukumu (Parquet) wanasema na uwongo juu ya kupata faida fulani. Lakini Mungu eko kule anasikia na atawalipiza wale watu. Na sasa sililizeni historia moja ya kweli.

Watu tatu walistaki Patriarche wa Jerusalema jina lake Narkissos.

Mtu wa kwanza alisema: Kama ninasema nwongo, ninaomba kwa Mungu anitumie moto iniunguze.

Mtu wa pili alisema: Kama ninasema uwongo, ninaomba kwa Mungu anipe magonjwa ya nguvu. Na ule mtu wa tatu alisema: Ninataka niwe kipofu kama ninasema uwongo.

Kisha hii kiapo yao, wale watu wa kuhukumu waliwasadiki, lakini Mungu akasirike juu yao, akawaazibu. Nyumba ya ule mtu wa kwanza ikaungua bila kujua sababu, na alikufa yeye pamoja na jamaa yake.

Ule mtu wa pili alipata magonjwa, aliteswa muda kidogo, na ku mwisho alikufa na maumivu mengi.

Ule mtu wa tatu, wakati aliona ile mateso waliteswa nayo ndugu zake wa wili, alitubu nguvu, alilia machozi mingi na alipofuka macho yake kwa ajili yao na aliteswa katika uzima wake wote.

Lakini hapa na waonyesha ya kama Mungu analipiza watu fulani, lakini hapa wote. Kisha lufu yetu itakuwa wakati wa kutengenaza mambo yetu yote pamoja na Mungu wetu. Ile wakati Mungu atatumika na haki yake.

### 2. - Zambi ya Kuiba. -

Sasa utangalia kama mikono yako iko safi. Ya kazi gani?

Ni kusema kama unaiba vitu fulani ao unafauya matendo fulani bila haki. Zambi haina paka kama unatosha vitu fulani vya ndugu yako, lakini tena kama unaiba makuta ya inchi

(l'etat) yako kwa kusema uwongo ao kutosha vitu fulani. Fahamu vizuri ndani ya akili yako, ya kama kila kitu uko nayo isipokuwa yako ni moto itakuunguza.

Kama watu wengine wataweka juu ya kichwa yako makala ya moto, utafanya nini? Utaitosha mbiombio. Fanya vile na sasa. Tosha na tupa mbali na mwili na uzima yako vitu vyote vya watu wengine, kwa sababu si vyako. Kama unakataa wakati moja Mungu atatosha vitu vyako juu ye kukulipiza. Kama unazola vitu fulani pasipo haki, pepo ya Mungu itafike na itavitupa inje pamoja na vitu vyako. Sasa sikia historia moja: Commercant mmoja alianza kuuza na kuuzisha nyusi ya kushona manguo. Pole-pole na hii kazi yake yasipo haki alifungua magasine na aliweka ndani vitu mbalimbali. Kisha wakati kidogo alifungua megasine ingine mingi. Alijenga ma nyumba marefu na depots munene. Aliuza mashamba. Watumishi wengi walitumika kwake juu ya kuuza yeye alikuwa na kipimo moja (balance), na kipimo ingine ya kuuzisha. Lakini yeye alitumika pasipo woga wa Mungu, pasipo kuwaza ya kama Mungu anaona yote. Ku mwisho ya uzima wake hakukuwa kitu hata kidogo. Ilibakia paka nyusi kidogo kama alivyokuwa ku mwanzo. Wakati alikufa hakukukuwa makuta ya kuuza mbao ya kumufanyia sanduku yake, na walitosha mbao tatu kati ya ile ilikuwa ya kabati ya magasine yake.

## 3. - Zambi ya machukizo. -

Tena, waza, kama mikono yako iliandika barua pasipo jina lako juu ya kuletesha sikitiko ao kuharibisha uzima ya watu wengine. Ao uliandika barua na mafundisho mubaya ya usharati. Hii kazi ni zambi kubwa, kwa sababu inaleta machukizo na kizibio ku wokovu wa watu wengine, kwani sababu ya hii tendo lako watu wengine wanapenda kutenda zambi ya usharati. Na Bwana Yesu Kristu anatuonyesha hivi: «Lakini ole kwa mutu yule anayeyaleta. Inafaa afungiwe shingoni jiwe kuwa la kusagia, apate kuzama kilindini mwa bahari' (Matayo 18, 6-7).

Tena mikono yako kazi gani inafanye? Hii kazi yako iko muzuri ao mubaya? Ni kusema utaokoa roho yako na hii kazi unafanya ao utaipoteza?

Kwa sababu Bwana Yesu Kristu, anasema hivi: Mutu atapata faida gani kama akiwa mukubwa wa dunie yote, lakini alipoteza roho yake? (Marko 8, 36).

Utangalia mikono yako, na ya wengine kama yanafanya zambi. Ni kusema, kama yalipita watu wengine, ao yalipenda kuua mwili yako: ao ndugu zako wengine, ao yalitumika juu ya kutosha mwanamuke mimba yake. Huyu mtoto wewe ulitosha na ulitupa ni mutu, wewe ulimuua na mikono yako, kwani uliwaza ya kama uko masikini na hauwezi kusaidia watoto wengi kuishi vizuri.

Ndio, inafaa kuzaa hapana watoto wengi kwani wao watateswa sababu ya njaa.

Ndugu yangu mupendwa, hii uzima tunaishi sasa ni matayarisho ya kuingia mu uzima ingine ya milele. Kwa mufano kama kwiko vita na waaskari wengine wanakataa kubeba bunduki, wakubwa yao, watawa na kwa sababu wanakataa uhuru wa inchi yao. Vilevile na kama bwana mmoja pamoja na bibi yake wakisikilizana juu ya kutosha mtoto yao ndani ya tumbo ya mama yake hawataingia mu ufalme wa Mungu. Biblia inatuonyesha ya kama mwanamuke ataokolewa kama atazaa watoto wengi. Mungu atakalipiza kama wewe unateswa ya kusaidia watoto wako kwa kukomea vizuri. Mambo yote ya mateso yako Mungu anaiona na atakulipa. Ya hii mambo wale watoto si wako, lakini ni wa Mungu. Agano Jipya kwa kinywa cha Yesu Kristu inatwambia: Musiite baba yenu mtu yoyote wa hii dunia, kwa sababu Baba yenu ni moja, aliye mbinguni. Mungu alikuweka wewe sawa Mulinzi wa wale watoto wako.

Kwa mufano: Wewe unaacha watoto wako kwa ndugu yako, na huyu anawaua wote! Ni mubaya sana. Ni vile unafanyishisha avortement (kutosha mtoto mu mimba ya bibi yako. )

Tena utangalia mikono yako kama inasaidia ndugu zako masikini na mapendo ao hapana. Kwa sababu Biblia inatuambia: Mungu atakataa kutupatia wokovu kama sisi tunakataa kusaidia ndugu zetu.

## 3. - Mwenendo yako. -

Miguu yako inaenda wapi kila siku? Unaenda mu kanisa siku ya Mungu (dimenche) na siku Kuu kubwa ya Watakatifu yetu? Haujuwe ya kama mutu mmoja hapendi kuomba mu nyumba yake, yeye mwenyewe, ao mu Misa pamoja na ndugu (waminifu) zake ni zambi?

Hii kazi ya kuomba mu Misa ni lazima kabisa juu ya wokovu wetu. Kanuni moja ya mukutano Ikumeniki ya sita inasema hivi: «kama mwaminifu mmoja asitake kwenda ku Misa juma tatu (3) (dimanche), Mungu atamulipiza na mafingo ya nguvu». Unasikia ndugu yangu? Mafingo ya nguvu Mungu atakulipiza.

Halafu, unaenda wapi katika masiku ya Mungu na masiku kuu ya Watakatifu? Unaenda kutumika, kuuzisha mu soko? Lakini unavunja amri ya Mungu yenye kutuonyesha hivi: Utatumika paka masiku sita, utafanya kazi zako yote lakini siku ya saba utajitolea katika maombi kwa Mungu wako. Ni vile anasema Mungu katika Agano La Kale.

Siku moja Muhubiri mmoja aliwahubiri wale watu hawapendake kwenda ku Misa, aliwaonyesha historia: Siku moja mtu mmoja mutajiri alitembea alikutana na mutu mmoja masikini. Akasumbulia naye, alisikia mateso yake na alimupatia makuta mbili. Makuta yote alikuwa nayo ilikuwa saba (7). Kisha wakati kidogo, walitembea pamoja na ule mutu masikini, huyu alimuonyesha tena mutajiri mateso yake ingine, na ule mutajiri alimupa na makuta ingine mbili(2). Sasa ule mutajiri alibaki na makuta tatu. Wakafika pamoja ku chemchem moja walikula ile chakula alikuwanayo ule mutajiti, na kwa mazungumuzo yao alimupenda sana, mara ingine tena alimupa makuta ingine mbili (2). Ni kusema makuta yote alimupa ilikuwa sita (6), na yeye alichunga paka moja.

Lakini mara moja ule masikini aliamuka, alimukamata na mikono yake ule mutajiri juu ya kumuua.

Alitosha kisu na aliomba makuta ingine moja. Halafu, Muhubiri aliuliza wale watu walisikia mahubiri yake:

-Malipiza gani inafaa kulipiza ule mutu masikini mabaya? Kwa sababu yeye alipokea makuta sita (6) na aliomba na kisu ya ule mutu mutajiri na likuta yake ingine moja.

-Lufu, lufu walipaza sauti wakisema wale watu walimusikiliza.

-Ee, ndugu yangu, ni Mungu alawauwa ninyi. Kwa sababu Yeye aliwapa ninyi siku sita kila juma kwa kutumika kazi ya maisha yenu, lakini ninyi munataka kubeba na siku yake ya saba, ni kusema siku ya Mungu sababu ya kufanya kazi mbalimbali na munakataa kuingia mu Misa.

Tena ndugu yangu unapashwa kusopoka na kitu ingine moja. Unaenda ku magasine ya zambi kunywa pomba (lutuku, vinyo, biere), unacheza na papier ya makuta, ao unalewa? Inafaa kujua ya kama watu walevi, kama inavyosema Agano Jipya, hawataweza kuingia mu ufalme wa Mungu.

Kumbuka tena kama miguu yako ilienda kwa mufumu (mulozi). Kanuni moja ya mukutano Ikumeniki ya sita inakatazwa sisi waorthodiksi kwenda kwa mulozi, kwa sababu hii ni kazi ya shetani. Ushuhuda wa dawa yote ya mulozi inatoka kwa shetani ni hii: Kama kwa mufano itaonekana nguvu ya Yesu Kristu, mambo yote ya shetani itakimbilia mbali sana.

Siku fulani, mulozi moja pamoja na walozi wengine aliita roho fulani ya shetani, lakini zile roho za shetani hazikumujibu na hazikuonekane.

Alisikia paka sauti moja na ikamujibu na hasira mingi na kusema: Hatuwezi kufika karibu yenu, kwa sababu mwingine mmoja ameingia leo katika myumba yenu. Ule milozi alienda mara moja ku nyumba ya mama yake aliyekuwa muzee akamuuliza ni nani aliingia leo ndani ya nyumba yangu?

Mama yake alimujibu: Namna gani mimi nitapumuzika kila usiku, kama wewe unaleta hapa ma shetani yote na wanafanya makelele?

Jana nilileta Padri yetu Orthodoksi, mmoja alifanya sala: Maji ya baraka (Agiasmos) na nilipata ukimya yangu.

Tangu ile wakati ule mulozi aligeuza uzima wake. Alitubu kweli, aliacha hii kazi na dawa ya shetani na alifwata Kanisa Orthodoksi.

Pasopo, ndugu yangu, ni zambi kubwa sana kama uko na mambo moja na unaenda kwa mulozi juu ya kukusaidia. Kumbuka, wakati ulibatizwa, ulisema kwa Mungu, ya kama utatocha shetani na kazi yake yote utumishi wake, na utaishi pamoja na Yesu Kristu. Lakini, kama unaenda kwa mulozi, unafwata shetani, unakataa Mwokozi wa roho yako, Bwana Yesu Kristu.

## 4. - Macho yako. -

Kwiko namna kwa kila mutu kufanya zambi na macho yake, kama, kwa mufano, anaona vitu fulani ao anasoma, kitabu mbaya.

Tena kama anaangelia television na hii mapicha yenye kulete haya ku roho yake. Ni hivi inakuya pole-pole lufu ku roho, na neema ya Mungu haitaonekana. Biblia ya Mungu inatuambia ya kama macho yetu inaleta lufu ku roho, kama hatusopoke. Bwana Yesu Kristu anatuonysha hivi: «Kila mutu anayetazama Mwanamuke kwa kumutamani, amekuisha kuzini naye moyoni mwake» (Matayo 5, 28).

Ni kusema, kama mutu mmoja anamutazame mwanamuke mmoja na mawazo ya usharati, hivi anazini naye ndani ya roho yake.

Leo watu wengi wanaenda kuangalia television paka juu ya kupata zambi rohoni mwao. Kanisa yetu, lakini, inatushauria kusopoka na macho yetu kwa sababu kwiko namne ya kutenda zambi ya kwanza na akili na kisha na mwili yetu.

## 5. - Masikio yako. -

Kisha utaangalia masikio yako, kama unaweka sikio lako kwa kusikia kwa siri, ao wimbo mubaya ya dunia ao sauti mubaya ya watu wengine.

Tena utaangalia kama unatii wazazi wako na kuwaheshimu. Kwa sababu usivunje amri ya Mungu. Amri ya tano inatuambia hivi: Heshimu baba yako na mama yako, upate kuwa na miaka mingi mu hii inchi.

Unawaza deni gani uko nayo kwa wazazi wako? Ulikabula makilo ngapi ya mukate ulikula ku mikono yao?

Makuta ngapi wao walilipa kwa kukuuzia chakula, manguo dawa, kulipa waganga, vitabu, walimu na ingine-ingine?

Unaweza kuwarudishia vilevile vyote kama utaweza, halafu uwaheshimu na kuwatii. Lakini hautaweza kurudisha hii vitu vyote wazazi wako walikupa, kwa sababu hii maziwa ya mama yako ulinyonya hautaweza kumurudishiyo. Basi inafaa kuwaheshimu daima, wazazi wako. Juu Mungu aliwape wazazi uwezo wake wa kubariki ao kulaumu watoto wao.

Ile wakati ilianza vita ya pili mu dunia yote, ku mwaka 1940. Kijana mmoja mwanaume alipika baba yake. Ule baba yake alilia inje ya nyumba yake. Mtoto yake alipita karibu yake na alimuuliza: Juu ya nini unalia hapa sawa nyama ya pori? Ingia ndani. Halafu baba yake alimulaumu akamujibu hivi: «Naomba kwa Mungu huyu nyama ya pori atakukula wewe na hii nyumba yetu itabomolewa».

Kisha miaka kidogo ule mtoto yake alienda kuishi ku mugini ingine. Siku moja usiku ule nyama ya pori alirarua kondoo zake nyingi. Kisha akamuuma na huyu. Halafu atakumbuka hii laana (mafingo) ya baba yake alimulaanika zamani.

Alienda mbio kwa mganga mmoja na huyu alimuambia ya kama alipata ugonjwa wa imbwa. Kila siku alienda ku hospitali sababu ya kupata sindano. Lakini mukutembea tembea mu hii njia alipata baridi na likufa.

Nyumba yake ilibaki wazi bila mtu na kisha wakati ingine wa padri ya kanisa waliibeba na kule ndani ikawa fasi ya kufundishia kateshisme.

<u>6. - Roho yako. -</u>

Mara mingi sasa inapashwa kuangalia roho yako kwa sababu zambi mingi inaikaa ndani ya roho yetu. Sawa mu kioto. Ni kusema roho iko sawa centre ya zambi zote, na vitu vibaya. Hii zambi ni hasira na ukali. Bwana Yesu Kristu anatuambia: Mutu yoyote anayemukasirikia ndugu yake anapashwa kuhukumiwa» (Matayo 5, 22). Hii zambi inawahuzunisha watu, inapofusha macho ya roho yao na kuna namna wao kugeuka kuwa watu wengine. Zambi ingine mbaya ni chuki. Bwana Yesu Kristu anatuambia: «Lakini kama ninyi hamuwasamehe watu makosa yao, Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu vilevile» (Matayo 6, 15). Kwa mufano, sikilizeni hii historia: «Saprikios alikuwa Padri wa waminifu ile wakati wa zamani. Wafalme wa pagano wa Roma waliokombanisha Kanisa yetu. Ule Saprikios alikuwa na imani ya nguvu na mapendo kwa Mungu. Alitembea fasi yote kwa kushauria na kupatia nguvu wale wa kristiani walipenda kuteswa na kwa ajili ye Mapendo yao kwa Mungu. Tena yeye alipenda kufa katika mateso ya kuachana. Kweli, hii mapenzi yake ilitimizika.

Siku moja waaskari wapagano walimubamba na walimupeleka ku fasi moja sababu ya kumuteswa. Kijana mwanaume mwaminifu jina lake Nikiforos alimufwata mu hii njia, na alimuomba amusamehe mambo moja ya zamani.

Lakini ule Padri Saprikios hakutake kumusamehe. Mara nyingi Nikiforos alimuomba huruma, lakini Saprikios alikataa. Halafu mambo moja ya nguvu ilifanyika. Mungu alitosha neema yake mwa ule Padri, na wakati askari mmoja alikuwa tayari kumukata kichwa yake, Saprikios alimuuliza Juu ya nini unataka kuniuwa? Neema ya Mungu ilimutoka na asikujue juu ya nini alienda ku hii fasi ya mateso. Ku mwisho Saprikios alipoteza imani yake kwa Mungu, alisikitikia na kumukataa Bwana Yesu Kristu. Basi, ule kijana Nikiforos aliwaonyesha ya kama «Mimi ni Mwaminifu na nataka kufa katika mateso na kisu». Kwa hivi, ndugu zangu Nikoforos alipokea taji ya milele na utakaso jakini Saprikios, aliipoteza kwani alikataa ku samehe ndugu yake.

Tena utangalia roho yako kama unataka kukusanya vitu nyingi mu nyumba yako. Utachunga pake hii vitu uko nayo lazima. Ndani ya roho yako utaweka ya kwanza matakio ya kuokoa roho yako, hapana vile vitu vya dunia. Ndani ya roho yetu sisi tutaabudu Mungu, hapana makuta ao utukufu wa dunia, ao furaha ya bure.

Pasopo, tena muishi na unyenyekevu. Shetani halale anaweka mu akili na roho yetu mawazo ya kama sisi ni mukubwa kwa ndugu zetu na ya kama tunajua mafundisho yote ya dunia. Lakini hii majivuno Mungu anaichukia na atatosha ulinzi na mapendo yake mu roho na uzima yetu.

Zambi ingine kubwa kabisa ni usharati sawa ukoma, ilisambaa dunia kote. Hii zambi yote ya mwili ni haya mbele ya Mungu na ya watu.

Hii zambi yote ya usharati inamuondoa mtu mbali ya Mungu Mtakatifu na inaleta hasira yake. Ile wakati ya Noe, mu Agano la Kale, zambi ya usharati ilikuwa mingi, Mungu alisema hivi: «Haitabakia roho yangu (Nikusema mapendo yangu) kwa wale watu wanafanya zambi ya mwili».

Kisha alinyeshesha mvua ya masiku 40 na watu wote walikufa. Tena kwa ajili ya hii zambi Mungu alituma moto ya mbinguni iliharibu miji minene mbili: Sodoma na Gomora. Na, kwa sababu leo zambi ya mwili ni nyingi tutaongojea Mungu wetu kututumia maangamizi munene, kama tunakataa kutubu. Wale watu wa usharati hawataweza kuona Mungu. «Heri wenye moyo safi, maana wao wataona Mungu» (Matayo 5, 8).

Kitabu ya ufunuo inatuonyesha hivi: «Washarati na walozi watatupwa inje ya ufalme wa Mungu».

Tena zambi ingine ni kama tuko na imani kidogo na tunasikitika namna gani tutaishi kesho, keshokutwa na siku za mbele. Hii mambo inatuonyesha ya kama hatuna na matumaini ku mapendo ya Utatu Mtakatifu. Inapashwa kutumika kwa ajili ya maishe yetu, pasipo kuleta makelele ku roho yetu.

Tena utangalia ndani ya roho yako kama ulizarau ao ulikuwa na haya ya kuhakikisha inami yako kwa watu wakubwa ao kwa watu wengine mbalimbali. Muevangelisti Matayo anandika hii sauti ya Bwana Yesu Kristu: «Lakini kila mutu atakayenikana mbele ya watu, nitamukana vilevile mbele ya Baba yangu aliye mbinguni». (Matayo 10, 33).

Mwaminifu wangu kuiko namna ya kutenda ingine zambi ndani ya roho yako. Kwa hivi inafaa kusopoka kabisa juu mwili yako. Utangalia namna gani unaishi ndani na mbele ya jamaa yako, mbele ya kazi na watumishi wako.

Na hii kazi yako unasaidia ndugu zako ao hapana? Uko na roho ya mapendo; kwa sababu hata Mwokozi wetu alikuja katikati yetu kutumika hapana kutumikiwa na watu wengine.

Tena utangalia kama uliweka kufanye kazi muzuri ao ulikataa. Biblia Takatifu inasema: Ni zambi kama unawaza kufanya kazi moja muzuri na haufanye.

## KIPANDE CHA PILI.

## M A T U N Z O.

Unasema nini ewe Msomaji wangu? Ulitimiza mapashwa yako, kwani ulisoma hii kitabu? Hapana. Haukuitimiza. Ulisoma kwa kuangalia kama kwiko namna, vidonda vyote vya roho yako. Lakini pasipo matunzo vidonda vitabakia paka vile na vitaleta harufu ku roho.

Kwa hivi, kama unaisha kuona mambo yote ya roho yako, wende mbio kutafuta muganga. Na Muganga ni Padri wa roho. Kama, kwa mufano, unapata magonjwa fulani, utaenda mbio-mbio kwa muganga yoyote kukuponyesha? Ndivyo, utaenda wewe mwenyewe. Kwa hivi inafaa kuenda kwa Padri wa roho. Kama utaenda kwake utafungua roho yako wewe mwenyewe kwa Padri, na kwa Mungu. Nakuonyesha wewe mwenyewe utafungua roho yako, kwa sababu waminifu wengi wanaogojea Padri wa roho awaulize. Kwa hivi siku moja, Padri mmoja alivua Epitrahilio (nguo Takatifu, alivaa ku mwili wake juu ya kufanya hii fumbo ya Maungamo (Confession) na alimupatia ule mutu alifika kuungama.

Huyu mutu alimuuliza Padri juu ya nini unanipatia Epitrahili? Juu ya wewe mtoto wangu. Kwa sababu sasa vile wewe unafanya. Unakuwa sawa Padri na mimi nitakuambia zambi yote. Haupende kusema wewe mwenyewe zambi yako na unaongojea mimi nikuuliza mambo yako yote.

Muwaze mambo moja mutasema nini kama mutu mmoja mgonjwa ataenda kwa Muganga atakataa kumuonyesha fasi gani anasikia maumivu.
Halafu Muganga atamuuliza; Fasi gani uko na ma umivu? Ku licho, mukono, sikio, muguu, tumbo, kichwa? Na yeye (mgonjwa) atamuambia:  Mimi sitakuambia. Hii kazi utaifanya wewe, kwani wewe ni muganga.

Na hii mambo inafwatana na wale waaminifu wanaongojea Padri ya roho awaulize.

Lakini hii mambo haina Confession, ndugu yangu. Inafaa kusema wewe mwenyewe zambi zako zote moja-moja. Utaanza kusema kwanza zambi zako kubwa, pasipo kusikia haya, kwa sababu Bwana Yesu Kristu eko ndani ya hii fumbo na yeye atasamehe zambi zako.

Tena, inapashwa kusema mambo yako yote pasipo kimwambia Padri wa roho, kwa mufano, hii zambi fulani nilifanye lakini ni kosa ya mutu mwingine na si kosa langu.

Waaminifu wengi hawarendi ku beba uzito yote ya kosa ao zambi yao ku mabega yao, wanasema: ‘ Mimi sikukosa ni mutu fulani alinikokota kutenda hii zambi. Hapana. Kweli na muzuri ni hii: «Ndivyo Padri wangu, mimi nilifanya hii kosa (ao zambi). Haina muzuri kusema. Bibi yangu alikosa ao rafiki ao dunia muzima ilikosa.

Ndugu yangu, kwa hii maungamo utafungua kabisa roho yako na utatosha uchafu yote uko nayo ndani. Kila mutu ni huru kwa kazi yote ao zambi zake. Daraka ni kamili kwa kila mutu.

Ule mutu mwenye kuogopa Mungu na hapende kuvunja amri yake, dunia mzima haiwezi kumukokota. Mtakatifu Kosmas alishauria hivi waaminifu ile wakati aliishi: «Kama mbingu itanguka chini, kama inchi itaenda yulu, kama dunia yote itaharibika. Haiko mambo yenu. Kama maadui wataunguza mwili wenu ao wataikalanga, ao wataiba vitu vyote na mali yenu haiko mambo ninyi kusikitika. Inapashwa kuwapa; kwani haina yenu, Ninyi mukona lazima kabisa kabisa ya wokovu wa roho zenu kwa Bwana Yesu Kristu Kupita ya hii vitu vyote.

Dunia nzima haiwezi kubeba mambo haya yote mawili paka ninyi wenyewe kama munataka kuileta kwa mapenzi yenu.

Ndugu yangu, kama unapenda kupokea huruma na usamehe wa Mungu inapashwa kukumbuka zambi zote na makosa yako yote, na kwa machozi mengi utaomba huruma na baraka ya Mungu.

Pasopo kabisa ndugu yangu, peke yako hautaongojea kutengeneza zambi na kosa yako, nikusema ya kukataa kwa mufano, ku chambulana, kasirani, na mambo yako ingine, na kisha utaenda kuungama. Katika hii Fumbo utapokea zawadi mbili za Mungu: Utapokea usamehe wa zambi zako na nguvu (neema) ya Mungu juu ya kwendelesha mashindano yako ya roho.

Wakati gani utaenda kwa Muganga, kama kwa mufano uko mgonjwa? Wakati ugonjwa itaisha munyumba yako: Hapana vilevile na sasa kama uko na huzuni ya roho, kwenda mbio kwa Padri wa roho kupata matunzo.

Tena sopoka na mambo ingine. Hautaenda kuungama paka ile wakati wa kwarezima (Careme ya Paska) vile ya bure pasipo kitubio na utamwambia Padri wa roho: «Padri wangu unisomee mimi sala. Sikufanye hata zambi moja. Mimi ni tayari kupokea Komunyo Takatifu». Kama utafanya vile, ndugu yangu, hata ukiishi miaka mia moja hautaweza kuishi kidogo yulu ya maisha yako. Utanguka mara nyingi katika hii zambi ulitenda zamani, pasipo kwacha zoezo yako.

Hii siku ya kuungama inapashwe kuwa mwanzo wa uzima wetu mupya. Utakamata mipango na utasema hivi: «Kwa sababu Roho Mtakatifu ananipatia utakaso na usafi wa nafsi yangu, mimi nitakombana sababu ya kuchunga hii utakaso na baraka yake mupaka mwisho wa uzima wangu. Nitachagua mara 1000 kufa, hapana kuanguka mu hii zambi natenda mupaka sasa. Mara moja niliungua. Sitauungua mara ingine. Mara moja sikusopoke. Nilikunywa sumu ya zambi. Sitaweka tena ku kinywa changu. Mutakatifu Yoano Krisostome anatuonyesha: «Simba akiumia kidonda ku muguu wake hakuna namna kuumiwa kidonda kingine. Watu hawataweza kumukamata. Vile ndugu yangu, utakamata mipango na utaenda kuungama.

## KIPANDE CHA TATU. -

### Kwenda sasa kuungama. -

Ndugu yangu, usiongojee siku kuu mukubwa juu ya kwenda kuungama kwa sababu hautaende hata ile wakati kuungama unataka nikuambia juu ya nini hautaende?

Shetani anayekufunga wewe mupaka leo, atakuletea vizuio nyingi ukose kwenda. Shetani atakuonyesha katika mawazo ya akili yako, ya kama zambi zako ni kubwa ao hautaweza kuokolewa, ao Padri atasikitika na atakufokea kama atasikia zambi zako, ao shetani atakuonyesha ku masikio yako ya kama Mungu hatasamehe zambi zako. Lakini sopoka, wewe usimusikilize shetani. Zambi zote Mungu anaweza kuzisamehe. Pake wewe inafaa kufungua kweli roho yako kwa Mungu na kwa Padri wa roho na utakamata mupango ya kutengeneza roho yako.

Shetani atakuletea vita ya haya watu wengi shetani aliwafunga ku haya na hivi wao hawaweze kuungama zambi zao. Wale watu watanda kwa ndugu yao, ao kwa rafiki ao kwa jirani yao kuweonyesha zambi zao pasipo haya, lakini wakikaribia kwa Padri wa roho hawataweza kusema hata neno moja.

Weko na haya. Ndugu yangu, Padri wa roho ni mugeni, ni mara ya kwanza kukuona wewe. Tena yeye tangu ile wakati alipata uwezo wa kuunganisha aliapa ya kama kila zambi atasikia, ataiweka ndani ya kaburi ya roho yake. Hakuma baraka ya Mungu na ya Kanisa yetu kuwaambia watu wengine zambi za watu.

Tena hii zambi haupendi kusema juu ya haye, yote itaonekana kwa Mungu ile siku ya hukumu. Itaonekana kwa watu wote na kwa watakatifu, na kwa Malaika wa Mungu. Utakuwa wapi ile wakati, ee ndugu yangu, sababu ya haya yako?

Shetani ao watu wabaya weko na namna ya kukuambia: Fanya Confession mbele ya Ikone ya Yesu Kristu, ya Mzazi- Mungu na ya Watakatifu Wetu.

Lakini, mwaminifu wangu, unapashwa kujua ya kama kile Ikone haina ya kusamehe zambi. Yesu Kristu hakuseme ya kama Ikone itafungua zambi zetu na ita fungua na kule mbinguni. Hii maneno Bwana Yesu Kristu aliwaambia Mitume wake: Wowote mukiwasamehe zambi; zinasamehewa kwao, na wowote Mukiwafungia zambi zinafungwa kwao» (Yoane 20, 23). «Vitu vyo vyote munavyofunga duniani vitafungwa mbinguni: na vitu vyo vyote munavyofungua duniani vitafunguliwa mbinguni» (Matayo 18, 18). Mapadri ya roho wanaendelesha hii fumbo (mistere) walipokea Mitume wa Yesu Kristu.

Kuiko namna shetani kukuambia ku masikio yako ya kama zambi zako ni ndogo, si lazima kuungama. Pasopo, kwani ni miteko yake, juu ya kuungama wakati ingine. Ole, kwa jina la Mungu! Kama utawaza: «Nitaungama kisha mwezi moja», hata ile wakati, hautaweza kuungama. Shetani ni mwovu. Anataka kukataza wewe kuungama zambi zako, hii wakati wa sasa, eko ku mikono yako na anakuaga wakati ingine ya mbele. Lakini nani anajua, kama sisi tutaishi kesho ao kisha mwezi moja? Paka Mungu peke yake anajua. Na kama sisi tutakufa siku moja mbele, faida gani tutapata, kama tutapoteza uzima wa milele?

Na sasa musikie historia moja: Zamani katika inchi ya Russia mutu mmoja alitumika mu station ya mashua juu ya kufungua njia sababu ya mashua kupita njanja ingine kwa kuepuka msiba. Siku moja ule Mutumishi alicheza muchezo ya kartasi pamoja na watu wengine. Mtu mmoja alimuambia: Amka ufungue njia ya station, kwani saa ya kupitisha mashua ni karibu. Yeye alijibu: Acha, niko na wakati. Lakini, ile wakati yeye alienda kufungwa njia alikuwa amekwisha kuchelewa. Alipitisha Mashua na ilianguka yulu ya ingine. Ku kafanyikwa msiba kubwa, watu wengi walikufa. Wengine waliumiwa vidonda nyingi.

Ule mutumishi akapoteza akili yake na akazungukazunguka njiani na kusema: «minute moja tu, minute moja tu». Ni kusema sababu ya minute moja tu alipitisha Mashua inanguka, watu wengi wanakufa.

Sopoka na wewe Msomaji wangu. Si vizuri kugeuza ile siku unakamata mipango ya kuungama, kwa sababu kwiko namna ya kupoteza wokovu wako ku uzima wa milele. Na kisha hakuna namna ya kutubu.

Ile siku na saa, mupendwa ndugu yangu, tutaenda kwa Mungu kuhukumiwa juu ya matenda yetu, hatujue wakati gani itafika hii mambo.

Kwa hivi Mungu anatuambia: «Tazama sasa ni wakati wa Mungu kupokea maungamo yetu, sasa ni siku ya wokovu». Sasa inapashwa sisi kukanyanga shetani na kutosha mawazo yake yote na tutaenda kupata Padri moja wa roho.

Unawaza furaha gani utasikia na wewe na ndugu zako, na furaha gani watasikia Watakatifu na Malaika wote mbinguni?

Bwana Yesu Kristu anasema hivi: «Kuna furaha katikati ya Malaika wa Mungu juu ya mwenye zambi mmoja anayetubu» (Luka 15, 10).

Hii furaha ya roho mara ya kwanza utasikia wewe ndani ya roho yako. Unatafuta furaha na amani duniani hautaweza kwa sababu ni uwongo, ni furaha ya shetani dakika ndogo tena inajaa uchafu na zambi.

Hii furaha ya hii dunia inakuletea siku zote huzuni moyoni mwako, na hii sikitiko itakuweka mu moto ya gehena. Halafu, ndugu yangu, kwenda kile mara kwa Padri wa roho kutosha uchafu yote ku roho yako, kumuuliza mambo yako, na utapata amani, roho safi, neema ya Mungu na kitumaini ya uzima wa milele. Amin.

# K I T A B U YA TATU

## WAKATI GANI NI NAMNA KUPOKEA KOMUNYO TAKATIFU).

Juu ya nini inaitwa Komunyo: Mutu wa kwanza ndani ya Paradizo kule Eden aliishi katika ushirika na Mungu. Hii ushirika ilileta furaha mingi kwa watu wa kwanza. Lakini ilifika wakati moja ile ushirika katikati ya Mungu na mutu iligaribika. Kwani zambi iliwatenganisha watu wa kwanza na Mungu sawa ukuta. Hii matenganisho inaonekana mara ya kwanza kwa neno la kitabu cha Mwanzo: «Wakasikia kishindo cha Bwana Mungu akitembea bustani wakati wa upepo wa mchana nao mtu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asipate kuwaona» (Mwanzo 3, 8).
Ile matenganisho ilifanika ilikuwa kubwa na Mungu alitosha wale watu wa kwanza mu Paradizo ku furaha na ushirika walikuwa nayo pamoja na Mungu.

Walipowekwa mbali na uzima wa Mungu, wale watu, sawa anavyotuambia Mutume Paulo: «Ufahamu wao uliotiwa giza, waliotengwa mbali na uzima wa Mungu kwa sababu ya ujinga ulio ndani yao, sababu ya ugumu wa moyo» (Efeso 4, 18).

Ile ushirika katikati ya Mungu na mutu, ilikaribika kwa ajili ya zambi ya mutu wa kwanza ndiye Adama. Hii ushirika ilikuwa mara ingine na Bwana Yesu Kristu, Mwana na Neno la Mungu. Mutu aligawanya hii ushirika pamoja na Kristu, lakini Yesu Kristu tangu ile wakati alichukua Mwili na alikuja katikati yetu kuunganisha watu wote.

Ushirika wa Mungu mu dunia ni tendo la ushirika. Mtakatifu Mtume Paulo anasema: «Basi, kwa sababu watoto wameshiriki Damu na Mwili, yeye mwenyewe vivyo hivyo alishiriki kama wao. Hata kwa njia ya kufa apate kuharibu yeye aliyekuwa na nguvu za kufa, ndiye shetani» (Waebrania 2, 14). Ile Mwili alichukua Bwana Yesu Kristu ni Mwili kweli wa mutu, lakini pasipo zambi. Ni Mwili kamili na takatifu. Hali kimutu ya Yesu Kristu ni takatifu kamili, kwa ajili ya ushirika wake pamoja na hali yake ya kimungu. Halafu Mwili wa Yesu ni Mwili wa Mungu na Damu yake ni Mwili ya Mungu (Matendo 20, 28).

Mapendo ya Mungu, sawa vile inafunuliwa katika fumbo ya kuja kwake duniani sawa Mungu na mutu, ni kubwa. Tena Mapendo ya Mungu sawa inavyoonekana katika fumbo ya Komunyo Takatifu, ni kubwa.

Fumbo ya kwanza ni namna Mungu alijifanya mutu sawa sisi pasipo zambi. Fumbo ya pili ni namna mutu anaungama na hali kimungu ya Yesu Kristu. (2 Petro 1, 4). Katika Fumbo ya kwanza Mungu alikuja na unyenyekevu mingi katikati yetu, lakini katika Fumbo ya pili kila mutu anapanda ku fasi ya Mungu, mbinguni. Sisi tunashariki na Mungu, kwa sababu yeye ku mwanzo alishariki na sisi.

Katika hii Fumbo ya Komunyo na sisi wote waaminifu Orthodoksi tunasharikiana pamoja, kwani tunakuwa Mwili mmoja pamoja na Bwana Yesu Kristu, tunafanywa kuwa Mwili mmoja wa kiroho pamoja na ndugu zetu Orhtodoksi. Mutume Paulo anatufundisha hivi: «Kwa sababu sisi tulio wengi ni Mukate mmoja na Mwili mmoja: Kwa sababu sisi sote tunapokea sehemu ya ule mukate mmoja» (I korinto 10, 17).

Kwa hii Fumbo Komunyo Takatifu inawapa waaminifu Orthodoksi Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristu. Katika sehemu ya sita ya Evangelio ya Mutakatifu Muevangelisti Yoane. (6, 51-58).
Bwana Yesu Kristu anatuambia safi mapendo yake ya kutupatia Mwili wake sawa chakula chetu na Damu yake kama kinywaji. Tena anatushauria ya kama ni lazima kabisa kula na kunywa Mwili na Damu yake kama tunapenda wokovu wetu na uzima wa milele. Tazama sehemu ya hii Evangelio: «Mimi ni Mukate wa uzima ulioshuka toka mbinguni, kama mutu alikula mukate huu, atakaa milele; na Mukate nitakaotoa ni Mwili wangu, nitakaotoa kwa ajili ya uzima wa dunia» (Yoane 6, 51).

Kwa hii maneno sisi tunaona faida gani iko katika Fumbo ya Komunyo Takatifu katika uzima wa waaminifu wote Orthodoksi. Mafumbo ingine inatupatia neema ya Mungu lakini hii Fumbo ya Komunyo Takatifu inatupatia Bwana Yesu Kristu muzima, ni kusema hii Mwili na Damu yake.

Hii fundisho ya Evangelio tulisema kidogo hapa juu Bwana Yesu alifundisha wakati wa ile muujiza alifanya wa kulisha watu elfu tano (5. 000). Katika hii muujiza aliwapa watu Mukate, lakini mara moja aliwafundisha tena wale watu ya kama yeye eko na Mukate ingine ya Kimungu, ni Mwili na Damu yake, na hii ni chakula cha kweli na cha kinywaji cha kweli. Watu wengi walikula hii Mukate na Mwili walishiba tumboni mwao. Waliacha Bwana Yesu wakati walisikia sauti yake ya kama sasa atawapatia chakula na kinywaji Mwili na damu yake. Kwa lakini Bwana Yesu Kristu hakusikitika. Tena, akawatambua wanafunzi wake na akawauliza: «Ninyi munataka kuondoka vile vile? Basi Simoni Petro akamujibu. Bwana tutakwenda kwa nani? Wewe una maneno ya uzima wa milele» (Yoano 6, 67-68).

Na leo watu wengi wanamuona Bwana Yesu sawa paka musaidizi ku mambo ya uzima yao. Wanasadiki ya kama Bwana Yesu Kristu alikuja katikati yetu kutengeneza vizuri mambo yote ya maisha yetu. Lakini Bwana Yesu Kristu alikuja kati yetu ya kwanza kutakasa moyo na uzima wetu katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Katika hii Fumbo ya Komunyo Takatifu tunapokea neema na utakaso wake. Tunaishi pamoja na Mungu wetu na pamoja na ndugu zetu.

Inje ya kanisa, pahali tunapokea neema ya Mungu katika Mafumbo yote hakuna namna ya sisi kuishi vizuri uzima wetu. Ni kusema hakuna namna mti kutoa matunda pasipo mizizi.

## CHAKULA CHA MILELE.

Bwana Yesu Kristu anatuonyesha ya kama ni lazima kupokea Komunyo Takatifu kwa sababu pasipo hii chakula nafsi yetu itakufa Mana (mukate) ya mbinguni inapita ile mana (mukate) walikula taifa la waebrania mu jangwa. «Baba zenu walikula mana (mukate) katika jangwa, wakakufa. Huu ni Mukate unaoshuka toka mbinguni ili yeye mwenye kuukula asife …. . Kama mutu akikula Mukate huu, atakaa milele (Yoane 6, 49-51).

Wale Watu Waebrania, ile wakati walirudia ku inchi yao mupendwe walikuwa lazima chakula, na Mungu aliwapa hii mana (mukate). Na sisi tunatembea kwa kufika mu Yerusalema ya mbinguni na tunahitaji chakula, Mungu anatupatia hii chakula chake cha utamu na cha mbinguni, ile chakula chake inatupatia nguvu na uzima wa milele. Hii ni Komunyo Takatifu katika ile mukate na vinyo tunapokea Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristu. Yesu Kristu muzima eko ndani ya Kikombe Takatifu.

Kwa hii Fumbo shetani analeta mawazo mbaya ku akili ya watu wengine wanauliza namna gani hii iko Mwili na Damu ya Yesu Kristu? Kwani sisi tunaona paka Mukate na Vinyo. Ni vile wanauliza wale watu walimuone Bwana Yesu ku uso. Namna gani wao kwa macho yao waliona mutu mmoja, namna gani Yeye alikuwa tena Mungu? Kama mutu mmoja anasadiki ya kama ku mukongo ya uso wa Yesu Kristu kulikuwa hali yake ya kimungu, huyu anasadiki ya kama ndani ya kikombe Takatifu anajificha Bwana Yesu Kristu.

Maulizo ingine ya wale watu weko na imani kidogo ni hii:
Namna gani Mukate na Vinyo inageuka kuwa Mwili na Damu ya Yesu Kristu? Hii kweli ni muujiza. Hatuwezi kusikia na akili yetu. Lakini tunaweza kusikia namna gani inafanyika Vinyo? Tuko na miti ya kufanya vinyo mingi Mungu ananyeshesha mvua. Ile miti inakunywa ile maji ya mvua, kisha miezi chache inatupatia matunda ya Vinyo. Namna gani? Ao namna gani hii majani mbuzi na kondoo wanakula inageuka kuwa maziwa? Ao

namna gani sisi tunakunywa Maziwa na hii chakula inageuka kuwa damu ndani ya Mwili wetu. Namna gani?

Ule anafa ya hii mageuzo ya ajabu, si ni Mungu wetu Mwenyezi, Yeye taweza kugeuza ile Mukate na Vinyo sisi tunamupatia kuwa Mwili na Damu Yake? Matendo yote ya ajabu inawezekana kwa Mungu Yesu Kristu kuifanya Komunyo Takatifu ni chakula cha mbinguni, lakini watu wengi wanakataa, kuikula. Kwa maombi yetu: «Baba yetu uliye mbinguni… tunasema: «Utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku». Watakatifu yetu wanatufasiria ya kama hii chakula ni cha Mwili wetu lakini fundisho ya Mungu ni Komunyo Takatifu.

Pasipo chakula cha Mwili kila Mutu hawezi kuwa na nguvu ku Mwili yake. Zaburi 103 (104) mustari wa 15 inasema: «Na Mukate unaleta nguvu ku Mwili yetu na Vinyo (Divai) ya kumfurahisha mtu moyo wake». Mwili wa Yesu Kristu inaleta nguvu ku moyo ya kila mutu na Damu yake inaleta furaha takatifu.

Ni kweli, wale waaminifu hawakule hii Komunyo Takatifu weko na njaa wanaishi sawa ule mutu mupotevu. Kumbukeni yeye aliwaambia ninyi katika roho yake: «Wa ngapi wa Watumishi wa Mushahara wa Baba yangu wanakule chakula na kushiba na mimi hapa minakufa kwa njaa? (Luka 15, 7).

Juu ya ninyi waaminifu wengi unakataa kukaribia ku Kikombe Takatifu kupokea Mwili na Damu ya Yesu Kristu? Ku hii ulizo tunapenda kujibu sasa.

## IMANI KU ILE FUMBO YA KOMUNYO TAKATIFU.

Shetani alifanya nguvu na aliiondoa waaminifu wetu ku Kanisa na hivi wao hawapendi kupokea Komunyo Takatifu juu ya kupata uzima wa roho. Watu wote wanapenda kutembea fasi yote na kula chakula yote, lakini hii chakula ya Mungu, Mwili wake hawapendi kuikula. Tena shetani anaweka giza ndani ya roho na akili ya watu, hivi hawaoni imani ya kweli na namna gani watakaribia kwa kupokea ile chakula Takatifu.

Kwa hii fundisho tutasoma ya kama shetani anaondoa waaminifu ku hii Fumbo. Kisha tutasoma namna gani shetani anaharibu mufano ya Mapadri Wetu juu ya kosa ya fundisho yao kwa ajili ya ile Fumbo ya Komunyo. Ushindi wa kwanza na shetani kwa waminifu wetu ni hii: Waaminifu hawasadiki hii Fumbo ya Komunyo Takatifu. Weko na imani ya vitu vingine vya bure, lakini hawasadiki ya kwamba hii Fumbo inatupatia uzima wa milele. Kwa mufano: Mbele ya miaka 10, Mutu mmoja alisema ya kama alipata dawa ya kutunza CANCER ( Kindonde ya hatari).

Alisema iko sawa uvumbi. Aliiweka ndani ya maji na kila mgonjwa kama ataikunywa, atapona. Wakati wale watu walikuwa na ile ugonjwa walisikia hivi, walibeba vyombo, walienda ku nyumba yake kubeba maji na sawa pamoja. Pasipo kumufahamia, pasipo kuuliza waganga. Walifwata mutu mmoja wa bure na walisadiki ya kama yeye anasema kweli na alipata kweli dawa ya Cancer. Lakini ni uwongo.

Mufano ingine mutu fulani ni mugonjwa. Hali yake iko nguvu, na iko lazima kumuweka damu ingine. Ile wakati ule mugonjwa hatauliza kama ile damu iko pamoja na damu yake kwa sababu anasadiki neno la muganga, la infirmier huyu alichagua aina damu ya fulani.

Mufano ya tatu Dada infirmiere anapana dawa fulani kwa mgonjwa. Ule mgonjwa atapokea atakunywa pasipo kuuliza kama ile dawa iko muzuri ao mbaya, kwa sababu eko na imani ya dada infirmiere. Wale watu wanasadiki watu wengine wa bure wa uwongo. Kwa mambo mbalimbali na hawasadiki Mungu mwenye Mwili kweli, kwa sababu Yeye alimwanga damu yake Msalabani juu ye dunia yote ipate uzima na wokovu wa milele.

Yesu Kristu aliyetupenda kuliko watu wote. Yeye anatuhakikisha, ya kama kwa ile Fumbo ya Komunyo Takatifu tunapokea kweli Mwili na Damu yake. «Yeye anayekula Mwili wangu, na kunywa damu yangu, ana uzima wa milele; nami nitamufufua siku ya

Mwisho. Kwa maana Mwili wangu ni chakula cha kweli; na damu yangu ni kinywani cha kweli» (Yoane 6, 54-55).

Ule mutu hasadiki ya kama Komunyo Takatifu ni Mwili na Damu ya Kristu, huyu hasadiki Kristu. Tunawafundisha ninyi kwa sababu watu wengine wanasema ya kama wanamusadiki Kristu, lakini kwa hii Fumbo ya Komunyo Takatifu weko na shaka hawasadiki 100%). Hawasadiki ya kama ndani ya Kikombe Takatifu muko Yesu Kristu Muzima, wanawaza ya kama vile vitu viko ndani ni mufano tu hapana Mwili na Damu ya Kristu.

Yesu Kristu alisulubiwa kweli kule Golgotha hapana sawa mufano. Damu yake ilimwangika kwa ajili ya watu wote wa dunia na ya wakati wote. Sawa vile kule Golgotha Bwana Yesu Kristu alitoa Mwili wake Muzima ili wenye ku mwamini wapate wokovu wao, vivyo hivyo katika hii Fumbo ya Komunyo Takatifu anajitoa wote mzima kwa waaminifu kama chakula na kinywaji kwa maondoleo ya zambi zao na kupata uzima wa milele.

Mutu kama anasadiki ku sadaka ya Kristu Msalabani, inafaa kusadiki na ku Komunyo Takatifu sawa sadaka ya kweli. Katika Kanisa yetu Mafundisho yote inapaswa kuyapokea paka na imani yetu. Kama mutu anasadiki miujiza ya Mungu, inapaswa kusadiki ya kama ndani ya hii Fumbo, ile Mukate na Vinyo sisi tunaleta mu Misa, inageuka kweli kuwa Mwili na Damu ya Kristu.

Kama mutu hasadiki Komunyo Takatifu, hataweza kusadiki Muujiza ya Mungu kuumba vitu vyote dunia hataweza kusadiki ya kama Mungu ni wa kweli.

Ushinidi wa pili wa shetani ni ya kama waaminifu wengi hawapende Komunyo Takatifu. Wale waaminifu hawakomunikake kila wakati, wanakomunika paka mara ine kila mwaka.

Wazaeni, mutu mwenye kusikia njaa kila siku anakula paka mara ine kwa kila mwaka. Kuiko namna kuishi ule mgonjwa aliye na lazima ya kupokea dawa yake kila siku lakini anakataa kuibeba ao anaipokea mara kidogo.

Kwiko namna kuishi ule mutu?  Sasa tutangalia juu ya nini waaminifu wengi wanakataa kukaribia kwa kupokea Komunyo Takatifu.

## 1. - Mambo yale hawajui. -

Hawajui ya kama ni lazima kila wakati kupokea Komunyo Takatifu. Wanasema hivi: Sisi tutakomunika mara tatu (3) ao mara ine (4) kila mwaka. Lakini hii kukomuika haina ya kweli. Zamani ilikuwa kweli wale waaminifu walikuomunika kila mwaka mara tatu (3) ao mara ine (4). Lakini kukomunika huku ni ya kujaa giza. Inapaswa kuondoa hii giza. Zamani wale watu walikuwa na moto ya mishumaa (bougies) sasa wote weko na moto ya elecrique. Lakini shetani aliwaondoa waaminifu mbali ya Komunyo Takatifu na anawaonyesha: «Sisi tulipata kukomunika mara ine kila mwaka, lakini Bwana Yesu Kristu anasema kula na kunywa Mwili na Damu yake kila wakati:  «Yeye anayekula mwili wangu na kunywa damu yangu ana uzima wa milele»  (Yoane 6, 54). Na Mutume Paulo anatwambia: «Twaeni, kuleni, huu ni Mwili wangu, uliovunjwa kwa ajili yenu, fanyeni hivi kwa kunikumbuka Mimi» (I Korinto 11, 23-25). Hapa Mutume Paulo anandika «fanyeni» ni kusema ya kufanya hii Fumbo kila wakati.

Wale watu wanakataa kupokea kila mara Komunyo Takatifu hawajue namna gani waliishi waaminifu ile wakati walishi Mitume wa Yesu Kristu. Waaminifu wa ile wakati ya kwanza walikuwa na Mapendo mingi ya hii Komunyo.

Kitabu ya Matendo ya Mitume inatuambia ya: «Walikuwa wa kidumu katika mafundisho ya Mitume, na kuishi katika ushirika na katika kuvunja Mukate na kuomba» (Matendo 2, 42). Waaminifu wa kwanza walikomunika kila siku. Ni vile inatuambia hii kitabu cha Matendo ya Mitume 2, 46-47); «Na siku kwa siku kwa nia moja waliingia hekaluni, wakivunja Mukate nyumba kwa nyumba, na kupokea chakula chao kwa furaha, na kwa moyo mmoja».

Tena hawajui historia ya Kanisa yetu, iliyo na zoezo ya kufanya kila siku hii Fumbo ya Komunyo Takatifu. Kwa hii mambo ile wakati wa Kwarezima (Careme) ya Paska tunafanya Liturgia ya Proigiasmeni, kwa sababu kuna waaminifu wanataka kupokea Komunyo Takatifu mara ingine katikati ya kila juma ya wakati wa kufunga. Ile wakatifu Yoane Krisostomos paka kila posho na mu juma. Liturgia Proigiasmeni inaitwa hivi kwa sababu Mwili wa Yesu Kristu ulitakaswa mu siku ya Mungu (Dimanche) ya nyuma.

Tena kanuni 8 na 9 ya Mitume yanatuonyesha ya kama, mutu anaenda mu Misa inafaa kukomunika. Kama yeye eko na mambo fulani inafaa amwambie Padri kama hakuna mambo na anakataa kukomunika. Kanisa itamupatia mafingo, nikusema kumufukuza ku Kanisa.

Tena wale watu wasipopenda kukomunika hawajue juu ya nini inafanyika ibada Takatifu ya Litugria. Hatufanye Liturgia sababu ya kusikia paka mwimbo fulani ao kusikia sauti ya mwimbaji ao Padri fulani ku Mwanzo tunafanya Liturgia juu ya kufanya katikati ya hii Fumbo ya Komunyo Takatifu.

Tena hawajue ya kama ni zambi kubwa kama mutu anaenda mu Misa na hapokee Komunyo Takatifu. Kama yeye alifanya zambi fulani ataungama kwa Padri wa roho yake, huyu atamuonyesha wakati gani atakomunika. Ni zambi kama hatupende kukomunika, kwa maana tunazarau Bwana Yesu Kristu. Padri anatuita hivi ku kila Liturgia: «Kujeni na woga wa Mungu, imani na mapendo…… «Lakini sisi hatukaribie. Leo waaminifu wengi hawajui ya kuwa ni zambi kama pasipo mambo, wanakataa kukaribia ku kikombe Takatifu. Shetani anafanya nguvu ili wale waaminifu waishi ndani ya giza ya roho.

## 2. - Unyenyekevu ya uwongo. -

Tunasikia mara nyingi waaminifu wanasema: Namna gani nitakomunika kila juma? Mimi sistahili. Mimi ni nani nikaribie kila juma ku kikombe Takatifu? Ni vizuri kama minakomunika katika sikukuu ya mwaka, nikusema sikukuu ya kuzaliwa, ya Ufufuo na siku kuu ya Kuzaliwa, ya Ufufuo na siku kuu ya Kulala Mama Mzazi-Mungu le 15 aout.

Hii maneno yao haiko maneno ya unyenyekevu. Mara ingine ni unyenyekevu ya uwongo. Ni unyenyekevu kwa maneno ya kama mutu mmoja anasema: Mimi si stahili kukomunika kila juma, paka mara tatu (3) ao mara ine (4) kila mwaka. «Sisi tunamuuliza, namna gani yeye anajua ya kama anastahili kupokea komunyo Takatifu mara tatu ao mara ine kila mwaka? Mbele ya Mungu hakuna mutu aliyestahili kuungama pamoja na Bwana Yesu Kristu katika Fumbo ya Komunyo Takatifu. Ni muzuri sasa kukumbuka hii maombi ya wimbo wa wakheruvi, anasema hivi:
«Mtu hata mmoja wa wale wenye kufungiwa na tamaa na furaha za mwili anayestahili kuja kwako kukujongea na kukuabudu ee Mfalme wa Utukufu……. ’

Tena ni vizuri kukumbuka sala moja ya Komunyo Takatifu: «Ee Bwana Mungu wangu, ninijua ya kama sistahili……. . ’

Hatukukomunika kwa sababu sisi tunastahili, lakini Bwana Yesu Kristu anapenda tumupokee akae ndani ya roho yetu. Hatukukomunika kwa sababu sisi tunastahili, lakini tuwe wenye kustahili.

Ninataka kukuliza wewe ndugu yangu mwenye kukataa kupokea Komunyo Takatifu, kwa sababu, unasema, hauna stahili: Siku gani moyo wako itakuonyesha ya kama wewe unastahili? Kama siku moja utasema sasa wewe unastahili, halafu utakuwa kupita msiyestahili wa yote mara ingine. Kama unaweza kukomunika ile sikukuu ya Ufufuo, ya Kuzaliwa Bwana Yesu Kristu, juu ya nini hautaweza kukomunika na kila mujuma? Maulizo yangu haya ni ya wale waaminifu wanapenda Komunyo Takatifu na wanatayarisha muzuri roho yao kila wakati. Kwa watu wengine hakuna kitu mimi sipende kuwauliza.

Komunyo Takatifu haiko zawadi ya utakaso wetu. Ni ya lazima ya roho yetu kupata nguvu ku uzima wetu juu ya kupata njia ya utakaso. Tazama, namna gani anaomba ule mwanimifu anapenda kupokea Komunyo Takatifu.
'Unirehemu, ee Bwana, nisiwe kama … nitimize amri zako'.

Tunakaribia ku Kikombe Takatifu kwani tunasadiki ku huruma kubwa ya Bwana Yesu Kristu na wema wake. Tunakaribia kwa kukomumika, kama tuko na baraka ya Padri wa roho yetu. Waaminifu wengi wanatuambia jibu lao lingine, kwa mfano:

1) Paka Mapadri wanaweza kukomunika kila wakati Komunyo Takatifu. Waaminifu hapana. Lakini juu ya nini hii mambo ya kuachana? Biblia Takatifu fasi gani inatuambia ya kama paka Mapadri weko na ruhusa ya kupokea Mwili na Damu ya Yesu Kristu kila wakati? Katikati ya Mapadri na waaminifu mbele ya Komunyo Takatifu hakuna achanisho. Wote wawili wanaweza kupokea Komunyo Takatifu. Wakati Padri anaomba kwa Mungu anasema hivi: Na unatustahilisha katika mukono wako wa nguvu kutupatia sisi Mwili Wako safi na Damu Yako yenye sifa na taifa yote.

Ni Mambo ya ajabu, kwani kuna Mapadri fulani wanazuia waaminifu wengine kupokea Komunyo Takatifu kila wakati. Mtakatifu Nikodeme anasema ya kama, wale Mapadri wanaita waaminifu kupokea katika. Woga wa Mungu, imani na Mapendo Komunyo Takatifu, na kisha wanawazuia wale waaminifu weko tayari rohoni wao kwa sababu wanapenda kukomunika.

2) Watu wengine wanasema ya kwamba paka kisha wakati wa kila kufunga (Careme) inapaswa waaminifu kukomunika kwa sababu ile wakati kwa mufano, wakati wa Paska ao wa Kuzaliwa Bwana Yesu Kristu watu wengi wanakaribia kukomunika.

Hii zoezo haiko ya kweli. Mtakatifu Yoane Krisostomos anatufundisha hivi: Paska ni kitu ingine, Kwarezima nayo ni kitu ingine. Kwarezima (wakati wa Careme) tunaifanya mara moja ao mbili kila mwaka. Lakini Paska (ile siku tutakomunika) tuko nayo mara tatu kila juma, ao mara ngapi sisi tunataka. Paska inafanyika hapana kwa ajili ya Kwarezima, lakini, ile wakati inafanyika sadaka ya Bwana Yesu Kristu mu Liturgia Taka. Tunashangilia Paska hapana wakati tunafunga (tunafanya Careme), lakini wakati tunapokea Komunyo Takatifu.

Ninajua, anasema ule Mtakatifu, ya kama waaminifu wengi wanaenda kukomunika paka Siku Kuu ya Paska ao ya Kuzaliwa kwake Bwana Yesu Kristu. Inapaswa, hapana paka kuangalia siku gani iko Siku Kuu fulani juu ya kukomunika, lakini kusafisha roho yao na kisha watakaribia kukomunika. Kwani, ule mwaminifu ni mwenye zambi, pasipo kutubu hata wakati wa Siku Kuu fulani ataweza kupokea Komunyo Takatifu. Lakini ule mwaminifu anasafisha zambi zake kila siku kwa kutubu na machozi yeye anastahili kukomunuka Siku Kuu yoyote na ku kila Liturgia anastahili kupokea zawadi ya Mungu (Komunyo).

Kila mara mwaminifu anapokomunika yeye eko na Paska ku nafsi yake (roho).

3) Wengine wanasema: Ni lazima kukomunika hapana mara nyingi juu ya kukaribia ku Kikombe Takatifu na heshima na woga mingi wa Mungu. Wanasema ni hatari kukomunika ni mara nyingi. Ni vizuri kukomunika mara kidogo, hivi tutasikia muzuri kabisa ushirika wa Mungu ndani ya roho yetu.

Hii mawazo yao haina ya kweli. Ule mutu mwenye kuheshimu na kuogopa kweli Mungu, ya kwanza anaheshimu neno la Bwana Yesu na Mapadri watakatifu wa Kanisa yetu wale wanatufundisha kukomunika kila wakati. Kama tunazarau maneno ya Mungu hakuna heshima kweli mbele yake. Hii heshima si kitu ya umutu. Ni zawadi ya Roho Mtakatifu. Na kama tunakomunika kila wakati atatupatia heshima na woga mingi wa Mungu na mapendo ya sala kwa ajili yake. Mwenye kustahili kabisa ni ule mutu anakomunika mara nyingi kwani anashindana na shetani hapana na nguvu yake, lakini na nguvu ya Mungu.

Eko pamoja na Mungu Mwenyezi. Lakini ule mutu anakataa, kwa mapenzi yake kukomunika, anakataa kuungama na Bwana Yesu Kristu. Vile eko mu hatari ya kuwawa

na imbwa ya pori, ni kusema, shetani. Ndio maana ule mwaminifu anapenda kukomunika, anaomba kwa Mungu akisema: «Sikuzarau lakini na kuomba».

Huyu mwaaminifu hajongee paka na zoezo ya bure. Hajongee kwa kuzarau hii Fumbo. Zamiri yake ni kuwa yeye ni msiyestahili, lakini anakaribia, kwani anasikia lazima rohoni mwake. Anakaribia kwa sababu eko na msingi wa rehema na mapendo ya Mungu. Anakaribia kukomunika kwani anaogopa shetani.

Wengine wanasema ya kama wakikomunika mara nyingi roho itakuwa na zoezo ubaya, lakini wanasahau ya kama Komunyo Takatifu ni ya lazima kabisa kwa ajili ya roho yetu.

Juu ya nini wanakula mkate (bukari) na wanakunywa maji kila siku pasipo kusema mwili wetu itapata zoezo mubaya? Tunajua ya kama pasipo Mukate (bukari) na maji mwili wetu itakufa. Lakini hii hatari iko na ku nafsi yetu, pasipo chakula ya mbinguni (Komunyo Takatifu) roho yetu itakufa.

Zoezo mbaya ni kweli iko lakini kwa watu gani? Kwa wale watu wanakaribia kukomunika pasipo kutayarisha roho yao. Wao kwa desturi wanakomunika moja ao mara myingi kila mwaka. Kwani ni wazazi wao waliwapatia sawa uriti. Wanakuja kukomunika kama ni zoezo yao.

Wale waaminifu wa kweli wanakomunika kila wakati. Kukomunika na woga na Matendo ya Mungu. Lakini hatari ya zoezo iko na kwa wale watu. Hii mambo inafanyikana ingine tena ya kuja ku Kanisa, lakini si vizuri kufika mu Misa paka mara mbili ao tatu kila mwaka kama ilivyo zoezo yao. Ao sala tutaifanya paka mara moja kila juma sababu ni hatari ya kupata zoezo, kama tunaomba kila siku? Haina vile, haina kweli. Tunakosea kila kazi ya roho, lakini si vizuri kusimamisha hii kazi ya Mungu.

Inapaswa kufanya nguvu kwa kutenda kazi yote ya roho katika woga na Mapendo ya Mungu moyoni mwetu. Kwa mufano, kila mara tunapoenda kupokea Komunyo Takatifu inafaa kuwaza ya kama tutakomunika mara ya mwisho. Komunyo Takatifu ni chakula kweli cha roho, ya kwanza kwa ajili ya uzima wa roho yetu na inafaa kuipokea na heshima na woga wa Mungu.

4. Wengine wanauliza kabisa Watawa ya jangwa hivi: Namna gani Watakatifu fulani walikomunika mara kidogo ao paka mara moja mu uzima yao lakini walitakaswa ?
Jibu ya hii ulizo inatoka kwa Mtakatifu Nikodimos wa Mlima Takatifu. Anatuambia hivi: «Kanisa yetu iliandika kanuni zake hapana juu ya Watawa ya jangwa, tena haiko Watawa wanaongoza kanisa yetu. Lakini kama Watawa wao wenyekupasha kupokea Komunyo Takatifu jangwani wanakataa kuikomunika wanavunja kanuni Takatifu na wanazarau Mafumbo yake. Lakini; kama hawakuweza kukomunika hawakuwa na daraka ya hii mambo yao.

Katika uzima ya Watakatifu, tunaona Watakatifu sawa Maria na Msiri aliyekomunika paka mara moja ku mikono ya Mutakatifu Mtawa Zosimas. Lakini hii ni mufano moja, ao mbili, ao tatu katika historia ya Ekklezya yetu, kanuni ya kufanya hii mambo watu wote.

Watawa Watakatifu wengine, sababu ya kuishi mujangwa mbali ya Kanisa, ao kule ku fasi hakukuwa Padri, hawakuweza kukomunika kila wakati. Lakini sasa tuko na Mapadri ya roho kazi yetu iko namna gani tutatayarisha muzuri roho yetu, tatafanya Confession na kama, tuko na baraka ya Padri, inapaswa kukomunika.

Hata bunduki moja ingine iko nguvu kupita sawa ile bunduki ya roho, nikusema, Komunyo Takatifu. Hata sala, hata Careme, hata sala ya usiku muzima iko yulu ya hii Fumbo ya Komunyo Takatifu. Bwana Yesu anatushauria safi sawa: «Musipokula mwli wa Mwana wa watu, na kunywa damu yake hamutakuwa na uzima ndani yenu» (Yoane 6, 53).
5). Watu wengine wanakomunika bila matayarisho, shetani anafanya nguvu kwa kuwakokota watu wengi wapokee Komunyo Takatifu pasipo matayarisho ya roho yao.

Komunyo Takatifu ni wokovu paka ya wale wanajitayarisha muzuri. Pasipo matayarisho Komunyo Takatifu ni moto, inatuunguza, na Mungu hakuna anatupa malipizi yake. Kama tunakomunika wenye kustahili tutaokolewa kwa sababu tunapokea dawa ya kuishi nafsi yetu milele pasipo kufa.

Tunapokea Matoleo ya zambi, ushirika pamoja na Roho Mtakatifu na tunapata uriti wa ufalme wa mbinguni. Kama tunakomunika pasipo woga na heshima ya Mungu tutapata malipizi ya Mungu kwani ni zambi kubwa.

Mutume Paulo anatushauria hivi katika barua yake ya kwanza kwa wa Korinto, Tazama maneno yake: '………. . 11, 27-30).

Hapa Mtakatifu Paulo anatuambia ya kama hatuwezi kukomunika na uchafu rohoni mwetu. Ni kusema bila hata matayarisho kidogo hii mambo ni kuzarau mbele ya Bwana Yesu Kristu. Kama tunazarau na tuko na uzaifu wa kutayarisha roho yetu hii ni zambi kubwa kabisa. Ndio maana katika hii chapitre ya yulu Mutume Paulo anasema: ' Kwa sababu hii wengi kwenu ni zaifu na wagonjwa na wengi wamekufa» (11, 30). Ni kusema, kwani walikomunika pasipo matayarisho, wengi waliapizwa kwa magonjwa na wengine walikufa.

Tulitazamia mwili wetu na mawazo yetu, kwa kutambua ya kama magonjwa mengi yanatufikia sasa ni sababu ya kukaribia ku kikombe Takatifu pasipo matayarisho? Tunawaza ya kama mara ingine watu wengi wanakufa kwa sababu wanazarau hii Fumbo Takatifu.

Ninawaza ya kama shetani ni mkali kwa namna mbili: ya kwanza hache waminifu kukomunika kila wakati juu ya mambo tuliandika mbele. Na ya pili shetani anawashauria watu wengine kupokea Komunyo Takatifu pasipo imani, pasipo mapendo, na pasipo kuungama rohoni mwao kwa ajili ya uzima wao. Tazama namna gani yeye (shetani) anawaonyesha:

-Kwenda sasa kwenda kukomunika. Wale wengine wanaenda kukomunika weko wazuri kukupita wewe? Si kazi nguvu. Utaenda mbio katikati ya watu wengine, utafungua kinywa chako, utakomunika, na mara moja utatoka mbio mu kanisa ……

Hii mambo sisi tunaiona kabisa kabisa mu juma Takatifu (Mu kazi ine na muposho mukubwa, na mu juma ya Ufufuo). Watu wengi wanaingia mu Misa, pasipo matayarisho ya roho yao, hata kufanya alama ya Msalaba pa kifua yao, wanakuja kwa Padri, wanakomunika na kisha wanatoka inje pasipo woga wa Mungu, wanaenda kuendelesha matendo yao mbaya na kumukufuru Mungu kwa uzima wao.

Daraka ya Padri ni kubwa sana kwa sababu anapana Mwili na Damu ya Yesu Kristu kwa wale watu wanazarau Mafumbo yote na uzima ya Kanisa yetu. Yesu Kristu anawashauria hivi: «Musiwape imbwa kitu kilicho kitakatifu, wala musitupe lulu zenu mbele ya nguruwe …. . » (Matayo 7, 6).

Tena weko na daraka kwa ndugu zao, wanawaambia kukomunika hata mara mbili kila mwaka, na wanaongeza ya kama ni vile iko zoezo mu kanisa yetu. Weko na wanawake wengine na wanalazimisha watoto wao (Mwanaume ao mwanamuke) kukomunika, na wanajua ya kama uzima yao si safi, imani yao haina muzima, mapendo yao ku kanisa ni bure. Wanawalazimisha na wakiwashauria hivi:

Mutii kwa kwenda kukomunika. Kama hamwende mitasikitika sana. Nitakufa juu ya sikitiko yangu …

Ni vile wanafanya na wanawake wengine kwa wanaume wao.

Enyi wa Mama na wa Baba, hii mapenzi yenu juu ya kuona watoto na ndugu zenu ya kupokea Komunyo Takatifu ni muzuri tena takatifu. Lakini namna yenu ni ya kuhukumu. Hii ni zambi kubwa sana ninyi hamujue. Musitende mara ingine hii zambi, kwa sababu munakosa juu ya wale watu wanapokea Komunyo Takatifu, pasipo kutayarisha roho yao. Komunyo Takatifu ni zawadi ya Mungu kwa wale waaminifu wanasadiki na wanagombana sababu ya kutakaswa.

Kila mara kwa kwenda kupokea Komunyo Takatifu ni lazima kutayarisha roho yetu. Mtu akitaka kula chakula mbele atanawa ku mikono yake. Hatakula chakula na mikono yake ya uchafu. Sasa, namna gani atafika mu Karamu ya siri na roho yake isiyo safi? Apana paka kwa kukaa lakini tena kwa kula Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristu. Halafu ni lazima kabisa kusafisha nafsi yake, kisha atakaribia kukomunika. Kwa mufano, kama mu nyumba yako unataka kushangilia, kufurahi kwa ajili ya Siku Kuu fulani, ao kupokelea mutu mukubwa mbele utasafisha na kuipamba na mapendo mengi kabisa utatayarisha ile fasi atakaa ule mugeni mutu mukubwa. Namna gani basi, utapokea nyumbani mwa roho yako ule mgeni mukubwa, ni kusema Bwana Yesu Kristu, pasipo kusafisha mbele nafsi yako na kifyakio ya kitubio ya kweli ? Safisha kwanza roho yako kwa machozi ya toba na kisha utakaribia ku kikombe Takatifu kupokea Bwana wa Utukufu wa milele?

Kila siku, tunafanya nguvu kwa kuchunga kanisa yetu safi, kwani ni ku hii fasi tunaabudu na tunatukuza Mungu wetu. Hatupendi kuacha Kanisa yetu, nyumba ya Mungu kuwa sawa nyumba ya wa nyama. Hatupendi hata mara moja kuacha wazi mulango ya Kanisa yetu, kwa sababu wanyama mbali wataingiamo, hivi Kanisa itaonekana sawa Kanisa ya sanamu pahali wanapotolea sakaka ya wanyama.

Hivi na roho yetu ni Kanisa. Inakuwa Kanisa kubwa ya Mungu, zaidi kama tunakomunika. Halafu ni kazi yetu ya kuchunga safi Kanisa ya roho yetu. Tutaisafisha kama tutaondoa zambi zetu na sanamu ya uwongo mawazo mubaya na kisha tutaenda kumupokea Mungu wetu Bwana Yesu Kristu.

Mapenzi ya Komunyo Takatifu inapaswa kuwaka ndani ya roho yetu sawa moto. Mbele ya kukomunika inafaa kutazamia mwili wetu. Kama moyo wetu inatuonyesha ya kama tulitenda zambi moja kubwa na hatujatayarisha bado roho yetu kwa kutubu si vizuri kukomunika, kwani ni zambi kubwa.

Sasa, namna gani inafaa kutayarisha roho yetu? Tutasoma hii fundisho itafwatayo.

<u>Komunyo Takatifu na kufunga (Careme). -</u>

Kufunga ni kweli bunduki juu ya shetani, lakini mara ingine hii bunduki shetani anaitumia. Nikusema, watu wengi wanafanya paka Careme (kufunga) na wanasema: ‘Tuko tayari kwa kukomunika; lakini hawako tayari’.

Sisi tutandika hapa hii fundisho inatoka ku kanisa yetu, hapana inatoka ku akili ya watu fulani. Ni kusema sasa tutafunza nini iliyo matayarisho ya kweli mbele ya kupokea Komunyo Takatifu.

Wale watu watakomunika paka mara mbili ao tatu kila mwaka, ni kusema sikukuu ya kuzaliwa na kufufuka kwake Bwana Yesu Kristu sababu walichunga vizuri uzima wa Kikristu, tukiwauliza:

-Mulitayarisha roho yenu ?

-Ndivyo, wanavyosema. Nilifunga siku tatu pasipo kula mafuta? Nilikula paka chakula pasipo mafuta? Wao wanawaza ya kama matayarisho ya roho ni paka Careme ya chakula. Kwa wao hivi walisafisha roho yao na wanastahili kukomunika. Kama, kwa mufano, tutauliza mtu mwingine mmoja hivi:

-Juu ya nini haufike kukomunika, yeye atatujibu hivi:

-Namna gani nitakomunika? Mimi siwezi kufunga. Ninatumika nguvu sana. Mimi siwezi kula pasipo Mafuta. Na yeye anawaza ya kama iko muzuri. Pamoja na roho yake. Kwa sababu hawezi kuchunga kula pasipo mafuta katika siku tatu, ni kule hafike kukomunika.

Hii mifano ya wale watu tunasema wanakosa sana. Kwani mutu mmoja alisema inaenea kufunga kula chakula bila mafuta siku tatu na kisha nitakomunika. Mwingine

alisema ya kama hawezi kuishi pasipo kula mafuta hata katika siku tatu. Ni kusema wote wawili walitenda mapenzi ya shetani.

Kufunga ni desturi ya zamani mu Kanisa yetu. Kwa mufano watu wa kwanza, Adamu na Eva nao pia walifunga walifanya Careme, na watu wakubwa wa Agano la Kale. Na tena mupendwa wa kufunga alikuwa ni Bwana Yesu Kristu Mwenyewe yeye alienda jangwani ajaribiwe na shetani «Akafunga siku makumi ine muchana na usiku, nyuma akasikia njaa» (Matayo 4, 1. 2). Tena Yesu Kristu anatufundisha ya kama kufunga ni bunduki ya nguvu juu shetani (Marko 9, 23).

Kufunga ni dawa ya nafsi yetu, inapaswa kuibeba ku wakati moja fulani, tuko na baraka ya Padri.

Wakati wa Kufunga (Kwarezima). -

Kanisa yetu inatuambia wakati gani tunafunga (Cereme) katika mwaka muzima tuko na siku za kufunga na siku zingine pasipo kufunga. Kwa mufano:

-Mukazi moja safi, na mujuma ya Apokreo ni Careme ya watu.

-Waaminifu wetu wote. Kama mutu mmoja anakula anakosa sana. Kila muposho (bila muposho mukubwa mbele ya Paska). Ni siku pasipo kufunga (Cereme), sawa vile inatwambia kanuni 64 ya Mitume.

Lakini kama mutu anafunga kwa mapendo yake ao kwa heshima ya Mungu, ao kama hajui, huyu hatende zambi. Lakini kama yeye anataka kusema nguvu kwa watu wengine juu ya kufunga ile siku, kweli anakosa sana.

Kanisa yetu inatufundisha ya kama Careme (kufunga chakula ) tunaifanya juu ya kutosha ku mwili yetu mawazo ya zambi ya usharati. Basi, ni lazima kufunga (Careme) juu ya macho yetu, ya masikio yetu, kwa sababu kufunga kwa kweli ni kabisa kabisa kuishi pasipo kutenda zambi. Kama tunafunga paka juu ya chakula, tunazarau Careme ya kweli; ni kusema ya kuondoa zambi zetu. Ndugu yangu, unafunga kweli?

Onyesha hii kazi yako katika makazi yako. Ni mawazo yako ya kuniuliza. Kazi gani nitafanya ya kuonyesha kwarezima yangu?

-Sikia: kama utaona mutu mmoja masikini, Umusaidie kama uko na adui yako umuonyeshe mapendo yako. Kama unaona ndugu yako mmoja mwenendo wake ni muzuri na mali yake na eko na cheo kubwa si vizuri kumuchukia. Inapaswa kumupenda na kumutakia, kama utaona mwenamuke mmoja ao binti, pita mbio mbele yake sababu usipate kikwazo. Tukifanya hivi tutafunga ya kweli na tutasifiwa. Wimbo mmoja tunaimba mu kazi moja safi inatufundisha hivi: Ninawatakia kufunga juu ya kumufurahisha Bwana Yesu Kristu. Kufunga kwa kweli ni kuacha matendo yetu yote mbaya, kuchunga nguvu ulimi wetu, kuacha hasira, kufukuza mawazo ya usharati, ya kuhukumu, ya kusema uwongo, kiapo ya uwongo. Hii yote ni kufunga kwa kweli, ya kuondoa zambi zetu.

Sasa kuiko namna ya kuangalia tafauti gani iko kati wa Komunyo Takatifu na kufunga (Kwarezima).

Wetu wengi wanawaza ya kama Kanisa yetu ilitupatia ile Kwarezima kubwa ine nikusema: ya Kuzaliwa Kristu, ya Kufufuka, ya Kulala Mzazi-Mungu na ya Mitume juu ya Kukomunika mara ine kila mwaka, kwa sababu mbele tunafunga.

Lakini tulisema mara nyingi ya kama Komunyo Takatifu haina paka mara ine kila mwaka. Ni chakula cha nafsi yetu, inafaa kuipokea mara nyingi. Pasipo hii chakula (Mwili na Damu ya Kristu) nafsi yetu itapata magonjwa na itakufa. Vile-vile hakuna tafauti hata kidogo kati ya Kwarezima kubwa ine na Komunyo Takatifu.

Mtakatifu Yoane Krisostome anatufundisha hivi: Ninaona waaminifu wengi wanakomunika paka na zoezo na sheria, hapana na roho na akili yao. Wanasema, ya kama, itafika wakati wa kwarezima (40 jours) wataweza kukomunika. Ni vile wanasema,

kwa ile wakati wa kufunga juu ya kuzaliwa Kwake Bwana Yesu Kristu. Lakini inafaa sisi kujua ya kama mutu fulani ni stahili hapana sababu ya wakati ya kufunga, lakini kama yeye atasafisha roho yake kwa ajili ya zambi zake. Pasipo hii matayarisho ya roho, hakuna namna ya kukomunika. Kwa zile siku Kanisa yetu inatuonyesha ya kwamba kwa kufunga inafaa kufunga kama tutaweza ao kama tunapenda, kisha tutakomunika ao apana.

Sasa, tunauliza: Kuna kanuni ya Kanisa yetu ya kufunga juu ya kupokea Komunyo Takatifu ?

Tunawajibu pasipo woga: Hapana. Mafundisho mengi sisi tunasikia ya kwamba mbele ya kupokea Komunyo Takatifu inafaa kufunga siku tatu kula pasipo mafuta. Lakini Mapokeo ya Kanisa yetu haiseme vile. Kufunga mbele ya kupokea Komunyo Takatifu ni mambo ya heshima na mapendo yetu.

Hakuna Kwarezima mbele ya kupokea Komunyo Takatifu: fundisho sisi tuko nayo ni hii:

Ya Kwanza Toka uzima ya Kanisa yetu ya kwanza. Hakuna fasi moja mu Agano Jipya na mu mafundisho ya Mapadri Apostolika inatuonyesha ya kama ni lazima kufunga mbele ya kupokea Komunyo Takatifu.

Ya Pili: Hakuna hata kanuni moja inasema kufunga mbele ya kupokea Komunyo Takatifu.

Ya Tatu: Tendo ya Kanisa yetu kama sisi tutapokea ile fundisho ya kuacha kula mafuta katika siku tatu, tutapata mambo kwani wale waaminifu wanapenda kukomunika kila wakati hawataweza kula hata kidogo Mafuta.

Ya ine: Komunyo Takatifu ya Mapadri. Mapadri yetu namna gani wanakomunika mara nyingi kila juma? Wanacha kula mafuta mbele ya siku tatu? Hapana. Ni vile namna na waaminifu kufanya. Tazama anasema nini Padri wetu mmoja mu ibada Takatifu (Liturgia): «Na unatustahilisha na mikono yako ya nguvu kutupatia sisi Mwili na Damu yako heshimiwa na katika sisi kwa watu wote».

Ndugu zetu wasomaji! Sawa vile ni zambi kama tutatosha kitu fulani ku fundisho ya Kanisa yetu, vilevile ni zambi kama tutaongeza fundisho moja fulani. Hii fundisho juu ya kufunga siku tatu pasipo Mafuta ilileta mambo mengi mu kanisa yetu. Kwani haiko ya Mapokeo yetu.

Ku Mwisho na wafundisha vile kwa wale watu wanakomunika kila wakati inenea ile Kwarezima Kanisa yetu inatupatia (nikusema mukazi tatu na mukazi tano, wakati ya Kwarezima ya siku zingine). Kama kwa mfano tutakomunika mu juma, muposho midi tutakula chakula na mafuta, na mangaribi tutakunywa chai, ao mukate kidogo na matunda. Kama Padri wa atamwambia mtoto yake wa roho kufunga siku fulani pasipo kula mafuta ile amri ni yake yeye Padri wa roho), haina ya Kanisa yetu na hakuna namna watu wengine kufanya vile. Hii ni malipizi Padri anamupa mtoto yake wa roho.

## Matayarisho ya kweli

Mupaka sasa tulisema ya kama watu wengi wanafanya matayarisho ya kukomunika paka kwa kufunga chakula fulani. Wanawaza ya kama, sababu walichunga wakati moja ya Kwarezima fulani, Walitayarisha roho yao kwa kukomunika. Na wanawaza ya kama wanastahili kukomunika lakini haina vile. Tunasema tena mara ingine ya kama Kwarezima na Komunyo Takatifu, ni vitu mbalimbali. Tunafanya Kwarezima hapana sababu tutakomunika, na tunakomunika hapana kwa sababu tulifunga.

Ni kweli ya kuwamba waaminifu hawatafika ku Kikombe cha Uzima pasipo matayarisho. Hawatafanya matayarisho ya teketeke, nikusema, kuacha kula mafuta siku tatu, lakini watafanya matayarisho ingine ya nguvu ya roho yao. Sasa tutandika Matayarisho gani ya kweli watafanya.

1. - Mapendo ya Komunyo Takatifu. -

Kama tunasadiki nguvu ya kama Bwana Yesu Kristu eko mzima ndani ya Kikombe Takatifu na ya kama hii chakula ni lazima kuikula juu ya kukomea roho yetu, hii imani inazaa roho yetu hamu ya kuipokea kila wakati. Wale waaminifu wa kiwanza ku Yerusalema «Siku kwa siku kwa nia moja waliingia hekaluni, wakivunja mukate ……» (Matendo 2, 46). Wao walikuwa na mapendo ya kukaa Hekaluni juu ya kukomunika.

Sisi tunataka kukutana wandugu yetu na jirani yetu katika mapendo mingi. Sasa anakuja katikati yetu Bwana Yesu Kristu inafaa kumupokelea na mapendo mingi kupita. Komunyo Takatifu haina paka tunakutana na Bwana Yesu Kristu, lakini tunaungana pamoja naye. Tunaungana katika Mwili na Damu yake na hivi Bwana Yesu Kristu atakuwa ndani ya mwili na katika uzima wetu.

Mapendo ya Komunyo Takatifu inakomea kama tunawaza ya kama pana hii tutabeba sawa uriti wa ufalme wa mbinguni. Mapendo yetu kukomunika ni mapendo ya Bwana Yesu Kristu. Njoo vile, mbele ya kukomunika tunasoma sala hii: «Kwa hamu nyingi napenda Kristu……»

2. - Kutambua roho yetu (hukumu). -

Wakati tunapenda kukomunika, inafaa kutambua mwili wetu, nikusema kama tuko tayari. Mutakatifu Paulo anatushauria hivi: «Lakini mutu ajihukumu Mwenyewe, na kisha apate kula mukate na kunywa Kikombe kwa sababu yeye anayekula na kunywa asipostahili, anakula na kunywa hukumu yake mwenyewe asipotambua mwili wa Bwana» (I Korinto 11, 28-29).

Tutatafuta fasi moja ya ukimya juu ya kuangalia ndani roho yetu, kama tunataka kukaribia Komunyo Takatifu. Ni kweli hakuna hata mutu mmoja anastahili 100% kwa kukomunika. Komunyo Takatifu haiko zawabu kwa watakatifu, lakini ni saidio kwa wenye zambi wenye kugombana juu ya kutakaswa.

Hatukomunike kwa sababu sisi tunastahili lakini juu sisi kuwa wastahili.

Hii kazi ya kujitambua wenyewe inatusaidia kuona zambi makosa ya roho yetu. Ule mwaminifu eko na hekima ya Mungu atatambua mwili wake kama kwa mufano mwaminifu mmoja roho yake inamuonyesha ya kama alitenda zambi kubwa, basi hataenda kukomunika. Ataenda mbele kuungama. Ile zambi iko hasira, zambi ya Mwili, fujo na makelele katikati yao.

Kama mwaminifu mmoja kisha kujitambua, anaona ya kama zambi zake tangu ile wakati aliungama mara ya mwisho ni kidogo na anasikia kweli ile zambi yake atakomunika.

Mtakatifu Anastasios, askofu wa Antiokia anatufundisha hivi: Kama tulianguka katika zambi kidogo, kwa mufano zambi ya ulimi wetu, ya macho yetu, ya majivuno, uzaifu, hasira kidogo mbele tutasikitikia zile zambi zetu, tutatambua mwili wetu na kisha tutakaribia kupokea Komunyo Takatifu. Mwili na Damu ya Mungu itatusaidia kusafisha zile zambi zetu. Kama tulianguka mu zambi kubwa, kwa mufano zambi ya usharati, ya kuchukia watu wengine basi inakatazwa kukaribia ku Kikombe Takatifu mupaka ile wakati tutatubu kweli kwa kuungama.

Ule mwaaminifu mwenye kuwa na baraka ya Padri wa roho yake kwa kukomunika kila mu juma, inafaa kuangalia roho yake. Kama roho yake inamuonyesha ya kwamba hakuna mambo aende, kukomunika basi yeye atafanya sala, na atachunga ile Kwarezima kanisa inatuoyesha. Ni kusema, kama mutu mmoja anakomunika na baraka ya Padri wa roho yake kila mu juma, hana lazima kuungama kila mara kama hakuna kitu.

Moyo safi 100%, hakuna namna kuipata, ni kwa hii mambo Komunyo Takatifu inasamehe zambi zetu ndogo. Kama sisi tunawaza ya kama tunastahili kupokea Komunyo Takatifu hii wazo ni majivuno. Watu wote hawastahili kukomunika. Tunakomunika kwa sababu tunatumainia rehema na huruma ya Bwana Yesu Kristu juu

ya kupata maondoleo ya zambi zetu, kuja kwa Roho Mtakatifu mu uzima yetu kwa kutupatia nguvu ya kuendelesha mashindano yetu juu ya kupata ufalme wa mbinguni.

### 3. - Maungamo (Confession). -

Kama roho yetu inatuonyesha ya kama tuko na zambi kubwa yenye kutuzuia kukomunika, inafaa kuungama.

Kama vile kwa kula chakula, mbele ni kunawa ku mikono yako, vivyo hivyo kwa kupokea chakula cha mbinguni ni lazima kabisa kusafisha nafsi yako na maji ya maungamo juu ya kupokea ile chakula.

Kila mwaminifu anasikia ile lazima ya kuungama zambi zake mbele ya kupokea Komunyo Takatifu kwa Padri wake wa roho ule mwaminifu anasema mara ingine maneno ya Mwana mpotevu: «Baba, nimetenda zambi juu ya mbingu na mbele yako, sistahili tena kuitwa Mwana wako» (Luka 15, 21).

Atamuonyesha Padri wake zambi zake zote na kulia machozi katika macho yake. Kisha atasikia Padri wake akimwambia: «Mwana, zambi zako zinasamehewa» (Marko 2, 5). Kisha maungamo furaha yake ni kubwa, kwa sababu aliokolewa ku sikitiko ya zambi zake, na tena kwa sababu alipokea baraka ya Padri wake juu ya kukomunika.

Ni mambo ya sikitiko kama waaminifu wengi ile wakati ya Siku Kuu kubwa wanakomunika pasipo kuungama. Ni mambo ya nguvu na ya woga, kwani watu wanakuja kukomunika, lakini katika uzima wao walitenda zambi nyingi pasipo kuungama.

Kazi nzuri ni kwa Mapadri wetu kuuliza waaminifu wetu kama waliungama na wakati gani, mbele ya kuwapatia Komunyo Takatifu. Watu wengine wanasikitika. Lakini juu ya nini kama muganga ni lazima kumupa mgonjwa dawa ya nguvu, mbele atamuuliza kama alijitayarisha. Vile basi, na Padri inafaa kuuliza waaminifu wake kama weko tayari. Hii maulizo Padri atawauliza waaminifu wenye kuja kukomunika paka mara mbili ao tatu kila mwaka, tena yeye anajua ya kama uzima wao ni mbaya, hawatubu.

Ni hivi inapaswa Padri kushauria waaminifu wake: «Ndugu zangu ninyi wote hamufike kuungama zambi zenu wakati ya mwisho na huruma na ruhusa ya Padri wa roho yenu, musikuje kukomunika. Ya kwanza inafaa kutayarishwa mwili wenu katika roho, kabisa kwa maungamo ya kweli na kisha mutakomunika.

Kama sasa hamuna wakati wa kuungama mutafanya hii Fumbo kisha Siku Kuu tuko nayo sasa. Kama muko tayari rohoni mwenu na munakomunika, muna furaha na sherehe katikati yenu. Munashangilia kweli ile sikukuu ya Kuzaliwa na Kufufuka Kwake Bwana Yesu Kristu, kama munastahili kukomunika. Kama mutakomunika pasipo kutayarisha roho yenu, mutaweka moto ndani ya roho na mwili wenu. Kwa sababu Komunyo Takatifu ni moto kwa wale watu wasiostahili. Nawaomba sana ninyi, mbele mutatayarishwa na kisha mutakomunika.

### 4. - M A P E N D O. -

Komunyo Takatifu ni tendo la Mapendo kwa ajili ya Mapendo yake mingi Bwana Yesu Kristu alikuja duniani na alitupatia Mwili Wake sawa sadaka ya wokovu Wetu. Ni vile anatuaambia Mutume Paulo: «Lakini Mungu akiwa mwenye rehema nyingi, kwa mapendo yake makubwa aliyotupenda sisi hata wakati tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu, alitupatia uzima pamoja na Kristo» (Efeso2, 4 - 5).

Bwana Yesu Kristu juu ya Mapendo yake mingi alikuja na aliungana pamoja na sili; kwa hivi na sisi inatupaswa kuungama pamoja naye katika Fumbo ya Komunyo Takatifu. Huyu Mwaminifu anayependa Bwana Yesu, anapenda kuzungumuza naye katika sala, anapenda kusoma kitabu yake, anapenda kumukula katika Fumbo ya Komunyo Takatifu. Kama anapoteza Mapendo kwa Kristu, hatakuwa tena na Mapendo ya kupokea Komunyo Takatifu.

Tena ni lazima kuwapenda watu wote kwa sababu Mapendo kwa watu ni ushuhuda ya kama tunamupenda Bwana Yesu. Mwanafunzi wa Mapendo, nikusema

Muevangelisti Yoane, katika barua yake ya kwanza anatufundisha mapendo tatu: mapendo ya Mungu kwa sisi, mapendo yetu kwake na mapendo yetu kwa watu wote.

«Sisi tunapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza. Kama mutu akisema: Ninapenda Mungu, naye anahukia ndugu yake, ni mwuwongo; kwa maana asiyependa ndugu yake aliyemwona hawezi kupenda Mungu asiyemwona. Na hii ni amri tumepea naye; Mwenye kupenda Mungu imemupasa kupenda ndugu yake vilevile» (I Yoano 4, 19 - 21).

Katika Mafundisho yake mulimani Bwana Yesu anatushauria ya kama mbele ya kuingia mu Misa inapashwa kusikilizana na ndugu zetu. «Basi kama ukileta sadaka yako mazabahuni na kule ukikumbuka ndugu yako ana neno juu yako, acha sadaka yako mbele ya mazababu, nende zako, kwanza patana na ndugu yako, kisha rudi utoe sadaka yako». (Matayo 5, 23 - 24). Ni vilevile na ku mwanzo wa sala ya Komunyo Takatifu tunasoma hivi: «Kula hii nitakayokula ……».

Na Mtakatifu Yoano Krisostome anatufundisha hivi: «Kama unachukia ndugu yako, hautaweza kupokea Mwilini mwako Mwili na Damu ya Yesu Kristu. Unataka kukomunika? Mbele utasikilizana na adui yako na kisha utakaribia kupokea Komunyo Takatifu'. Komunyo Takatifu ni mapendo na huruma kwa watu wengine wote. Lakini sisi tuko na majivuno na tunawaza hivi: «Juu ya nini nitaomba huruma; mimi sikukosa, ule alikosa ni yeye anapashwa kuomba wa kwanza huruma».

Hii mambo inatuonyesha ya kama hakuna unyenyekevu, hakuna masikilizano, hakuna mapendo. Pasipo mapendo hakuna namna ya kukomunika inavyostahili, kwa sababu Yesu Kristu ni mwenyi Mapendo. Na sisi tutamukaribia paka na mapendo. Muzuri ni mbele ya sisi kwenda mu Misa kupokea Komunyo inapashwa kuomba huruma kwa wazazi na ndugu zetu. Watoto wataomba huruma kwa wazazi wao, watabusu ku mikono yao na wataomba baraka yao.

## 5. - Sala na Matayarisho ya roho

Ule mwaminifu anapenda kukomunika mu juma atasopoka mingi sana mu uzima yake ku siku zote za mbele. Atafanya nguvu ya kutayarisha roho yake juu ya kupokea Bwana Yesu. Atasafisha roho yake na anasopoka juu asitende zambi. Ataomba kila siku, kabisa ile siku ya mwisho ili Mungu amustahilishe apokee mwili na Damu yake Yesu Kristu. Mu juma asubui ataenda mu Misa, ataendelesha kufanya sala na atasoma ku nyumba yake sala ya Komunyo Takatifu. Ile sala ya Komunyo inafaa kuisoma kwa wale wote wanapenda kukomunika. Ku mwisho ya hii ibada ya Komunyo kuna sala ingine ya kushukuru Mungu. Hii sala ataisoma kisha Komunyo Takatifu. Kuna zoezo ya kusoma hii sala ku mwisho ya Liturgia Takatifu waaminifu wote wanapashwa kuongojea juu ya kusikia hii sala ya kushukuru.

Ni mubaya kama watu wengine wanapokea Komunyo na wanatoka pasipo kusikia sala ya kushukuru Mungu. Wao wanafanana na wale watu wenye ukoma walionyeshwa na Bwana Yesu, lakini paka mu moja wao alirudi kumupigia Bwana Yesu Kristu 'AKSANTI'. Basi Bwana Yesu Kristu aliwauliza: 'Hapana watu kumi waliosafishwa ? Lakini wale tisa ni wapi? Hapana mwingine aliyeonekana kurudi kumupa Mungu utukufu ila mugeni huyu? (Luka 17, 17 - 18).

Ndugu zangu, munawaza kama mutu mmoja anamupatia mwingine zawadi yeye kisha kuipokea anatoka mbio-mbio sawa mwivi. Pasipo kumupigia mwenzake aksanti. Hii tabia yake iko muzuri ? Hapana. Ni vile na sisi, kama tunapokea Mwili na Damu ya Yesu Kristu tutaongojea Mwisho ya Liturgia sababu ya kusikia sala ya kumushukuru kwa furaha na sherehe na ushukuru mingi.

## 6. - Woga na Heshima. -

Matayarisho ya mwisho ni woga na heshima kwa Mungu. Padri atatuita hivi: «Na woga, imani na Mapendo ya Mungu mukuje». Ile woga inatoka kama sisi tunawaza ya kama tuko wenye zambi, tunasikia zambi zetu, tunasikia tunaenda wapi na tutapokea nini. Lakini ni mambo ya sikitiko kama ile siku watu wengi watafika kukomunika hawana woga na heshima ya Mungu.

Wanafika mbio mu Misa, wanafanya makelele ku mwisho ya Liturgia, wanapenda mbio-mbio kukomunika, wanasukumasukuma wenzao na wanasikitisha Padri na waaminifu wengine.

Mutakatifu Yoane Krisostome anatushauria hivi: «Juu ya nini ndugu yangu unakaribia ku Kikombe Takatifu pasipo woga? Uko na kisilani, unachambula watu wengine na unafanya fujo? Komunyo Takatifu ni Fumbo, na sisi inafaa kuikaribia paka na ukimya, heshima, na tabia yetu ya upole, kwa sababu tunaenda kupokea sadaka Takatifu. Hiyi kuna namna Mungu kutupatia mapendo na huruma yake; vile tutasafisha nafsi yetu na tutapata kwa Mungu vitu vya milele.

Inapashwa kusimama na woga mingi, na unyenyekevu, kuchunga macho yetu kuangalia chini, yulu tutafanya sala yetu na sauti ya roho yetu, kumwomba Mungu, kukumbuka zambi zetu na kulia machozi kama itawezekana. Hamuonake wale watu wanaenda kutazama mukubwa wa muji? Wasimama pasipo kuzungumuza, kimya pasipo kwangalia huku na kule. Zaidi sisi inapashwa kusimama mbele ya Bwana Yesu na woga, na mapendo, na heshima mingi. Mbele ya kukomunika waaminifu wanapashwa kufanya alama ya Msalaba, kisha watakamata kitambaa mwekunda wataweka chini ya kinywa yao, kisha watafunga muzuri kinywa chao, pasipo kutosha ulimi wao inje. Kisha kukomunika watapunguza kinywa chao, watafanya tena alama ya Msalaba na kisha wataenda pa fasi yao. Kule watakaa mupaka mwisho wa Liturgia sababu ya kusikia sala ya kushukuru Mungu.

## KIZUIO YA KUKOMUNIKA. -

Kizuio ingine ya waaminifu wetu kupokea kila wakati Komunyo Takatifu ni zambi zote za mwili. Kuna waaminifu wengi wanapenda kukomunika, lakini wanaguka katika zambi kubwa ya mwili, hawawezi. Kabisa vijana wanaume na wanamuke (ma binti) hawawezi kukomunika, kwa sababu mbele ya wakati kidogo wanatenda zambi ya usharati. Wanamuona Bwana Yesu Kristu ndani ya Kikombe Takatifu na wanasema ile neno la Mtume Petro: «Uniondokee, Bwana, kwa sababu mimi ni mutu mwenye zambi» (Luka 5, 8).

Wale waaminifu wetu weko na hamu ya kukomunika lakini mbele walizini, inapashwa kutafuta Padri mmoja wa roho. Wataungama kwake na yeye atawaambia wakati gani watapokea Komunyo Takatifu, kama wao wanatubu na wanaondoa mawazo yao mubaya. Pasopo mingi, kwa sababu watu wengine na vijana wanawaza hivi: ‘Nitatenda zambi fulani, kisha nitaungama na Padri wa roho yangu atanipatia ruhusa yake ya kukomunika.

Lakini hii mawazo ni kukufuru ile Fumbo ya kuungama. Padri wa roho atatupatia baraka yake ya kukomunika kama yeye ataona kitubio yetu na sisi tutasopoka kisha Komunyo kwa kuishi muzuri. Komunyo ni bunduki ya nguvu mbele ya shetani na ku zambi zetu.

Wale waaminifu waliunga ndoa wanaishi mume na muke wake, hawawezi kukomunika, kwa sababu kila wakati wanatenda zambi katikati yao. Kisha wanakataa kuungama, kwani wao wanasema: Padri wa roho yao atawazuia kupokea Komunyo Takatifu. Wanawake wengine wanatosha mimba (avortement), hivi wanauwa watoto wao. Hii zambi ya kuuwa watoto wao ni kubwa sana. Wao hawawezi kukomunika miaka mbili ao tatu.

Mapadri inapashwa kuwahubiri waaminifu wao kwa kutayarisha vizuri uzima na roho yao, na kisha watapokea Komunyo Takatifu. Waaminifu wetu wanapashwa kusikia ya kama pasipo Komunyo Takatifu wanaishi mbali ya nyumba ya Mungu sawa ule Mwana Mpotevu. Aliyesikitika na kuwaza hivi: «Wa ngapi watumishi wa wa Mushahara wa baba yangu wanakula chakula na kushiba, na mimi hapa ninakufa kwa njaa? » (Luka 15, 17).

Lakini ndani ya nyumba ya Mungu kanisa kuna chakula cha mbinguni cha Waorthodoksi wote, lakini wenyi kati yao wanakataa kuipokea, kwani hawapendi kuacha kutenda zambi zao.

Wakati Padri anakuja inje ku mulango mukubwa wa Ikonastasi na anatuita sisi kukaribia na woga na mapendo kwa kupokea Komunyo Takatifu sisi kama tuko tayari tutaenda. Bwana Yesu Kristu anakokola ku mulango ya roho yetu na anatuambia: ‘ Tazama, ninasimama kwa mulango, ninapiga hodi, kama mutu akisikia sauti yangu na kugungua mulango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami (Ufunuo 3, 20). Watu ngani weko na Mapendo ya kufungua mulango ya roho yao ? Kufungua kinywa chao kwa kupolea Yesu Kristu katika Mwili na Damu yake? Waaminifu wengi weko na mulango ya roho yao ya kufunga nguvu.

Inapashwa Mapadri kuhubiri sababu ya kuangaza akili ya waaminifu wao juu ya kupenda Komunyo Takatifu. Komunyo ni baraka munene kwa sisi. Ni sifa kubwa. Ule mutu anakomunika anaungana pamoja na Bwana Yesu Kristu na yeye anakuwa mtoto wa Mungu. Komunyo Takatifu inatupatia furaha na shangwe rohoni mwetu, kwani tunapokea kweli nguvu ya roho Mtakatifu. Tunapokea Bwana Yesu Kristu na tunamuita hivi: Mubarikiwa Yeye anayekuja kwa jina la Bwana. Bwana ndiwe Mungu naye amefunguliwa kwetu ……

Nawatakia waaminifu wetu wa mu Afrika kupenda Komunyo Takatifu juu ya kutakaswa na kuishi hii uzima na furaha mingi na matumaini ya kupata uzima wa milele. Amin!

MAFUNDISHO YA MTAKATIFU MUTAWA MAKARIOS

Kila Mutawa anapata wokovu wa roho yake kwa neema ya Roho Mtakatifu. Lakini ni lazima hii neema kusaidia ule mutu kwa matendo yake mema.

1. - Maulizo: Mapenzi ya Mungu ni nini, juu ya kila mutu kuitenda?

Jibu: Mapenzi ya Mungu ni kila mutu kusafisha kila zambi rohoni mwake, kuondoa kila wazo mubaya na kupata fazila ya Bwana Yesu Kristu.

Bwana Yesu Kristu anatushauria hivi: Heri wenye roho safi, kwa sababu wao wataona Mungu. Roho Mtakatifu anatushauria kuondoa rohoni mwetu zambi zote za zamani zinakomea ndani yetu sawa miti ya mizizi mirefu. Tutaziondoa kama tunafukuza mawazo mabaya kwa msaada wa sala ya Mungu, hivi tunapokea paka mawazo ya Mungu.

Inapashwa kuchunga vizuri roho yetu ku zile zambi kubwa zenye kuonekana, sawa usharati, kuuwa watu, kuiba, kula chakula mingi, kuhukumu watu wengine, kusema uwongo, tamaa mingi ya feza, kupenda utukufu ya dunia. Tena inafaa kusopoka na zile zambi ziko ndani yetu bila kuonekana, sawa matakio mubaya, utukufu wa bure, kupenda cheo, mkubwa kwa kupendezwa na watu, chuki, kujipendelea, majivuno, na ingine.

Kila kazi mzuri tunafanya inafaa kuifanya paka na utukufu wa Mungu, hapana wetu. Si vizuri kufurahi kama tunasikia neno nzuri katika uzima wa mwili wetu.

Pasopo na chuki. Mtakatifu Mwevangelisti Yoane anatuambia ya kama: «Ule mutu anachukia ndugu yake yeye anamuuwa». Mutume Paulo anatuambia ya kama mapendo inapokea yote, inavumilia yote, hakuna namna sisi kuanguka chini ya matendo yetu, inapashwa kuishi na woga wa Mungu na Mapendo Takatifu, hivi neema ya Bwana Yesu Kristu itakuja ndani yetu kama mutu mmoja hana na Mapendo na woga wa Mungu, basi huyu anatafuta utukufu wa dunia. Basi Yesu Kristu anatuuliza: «Namna gani ninyi munasadiki ya kama munapokea utukufu wa dunia Katikati yenu lakini hamuombe utukufu wa Mungu?

Inapashwa kuweka akili yetu ku sala ya Mungu, kwa kukumbuka jina lake, vile itazaliwa kwa watu wote kama chemchem: Mapendo, upole, unyenyekevu, wema, usafi na sala safi.

Shetani anafanya nguvu ya kuondoa katika akili yetu ile makumbusho ya Mungu. Anatukumbusha mambo yetu yote, sikitiko yetu, mambo ya chakula ya kesho, hivi sisi tutasimamisha kusali.

Pasopo kwa sababu zambi zote zinafungiwa sawa monyororo. Ni kusema, chuki inatoka ku hasira. Hasira inatoka ku majivuno, majivuno inatoka ku utukufu wa bure. Utukufu wa bure inatoka ku uzima wasipo imani. Uzima yetu wasipo imani inatoka ku roho yetu nguvu sawa jiwe. Roho yetu nguvu inatoka ku uzaifu. Uzaifu inatoka ku uzima wasipo uvumilivu. Na uzima wetu wasipo uvumilivu inatoka ku furaha ya Mwili.

Kama tunataka kufanya kazi moja nzuri kwa utukufu wa Mungu shetani anakuja anageuza mawazo yetu na tunafanya hii kazi kwa utukufu wa uzima wetu. Hivi sisi tunamutukana Mungu.

Mwanzo wa kupata fazila ni sala ya roho yetu. Kwa sala sisi tunapata ndani ya roho yetu shangwe na furaha ya kweli.

Bwana Yesu Kristu anatuambia: «Ufalme wa mbinguni unapatikana ndani ya roho yenu». Kwa hii mambo shetani anagombanisha kazi ya roho yetu, ni kusema sala, kwa sababu sala iko sawa moto yulu ya kichwa cha shetani. Kila siku tunapashwa kusali sala yetu na unyenyekevu mingi, na mapendo ya Mungu na ya ndugu zetu kama tuko na chuki fulani kwa ndugu yetu, Mungu hatapokea sala yetu.

Shetani anatuzuia sana wakati wa sala yetu. Analeta usingizi, uzaifu, uzito wa Mwili wetu, kugeuza mawazo yetu, makelele ku akili yetu anaondoa nguvu ya mwili wetu

na ingine. Kama tunaamuka na sala na hatupate unyenyekevu, basi hii sala tulifanya ni ya bure. Ni kusema fazila ya kwanza inazaliwa ku sala ni unyenyekevu.

Kisha ni amani, furaha ya roho, Mapendo …. .

Wale watu wasipoweza kufanya sala, inafaa kufanya kazi ingine, ya kusaidia watu, kutazama wagonjwa, na ingine.

Ule mutu anafanya sala si vizuri kujivuna ya kama ni yeye peke yake anasali lakini watu wengine apana. Kama mutu mmoja atasaidia wa ndugu zake si vizuri kusikitika kama ndugu zake wengine hawawezi kufanya sala.

Kama tunafanya sala kuiko namna shetani kutufikia sawa Malaika wa Mungu na taji kichwani mwake, lakini hataweza kutuletea furaha na amani, atatuletea paka woga na huzuni rohoni. Hivi inaonekana uso wake ya kama ni uwongo. Shetani anatuletea majivuno na majaribu mengi. Roho ya kila mutu itaweza kuona mwangaza yenye kutoka kwa shetani na yenye kutoka kwa Mungu kama inatambua yale matendo yake, ni kusema tukilikia woga ni kusema inatoka kwa Malaika wa shetani, lakini kama tunasikia furaha, unyenyekevu, amani, mapendo ni kusema inatoka kwa Malaika wa Mungu.

## Maulizo na Majibu

1) Kila mutu anapokea imani kwa nguvu yake mwenyewe, ao hii ni zawadi ya Mungu

-Imani ni zawadi ya Mungu (Roma 12, 3; Efeso 2, 8, Filipo 1, 20; 2 Petro 1, 1). Imani ni kazi ya Mungu (Matendo ya Mitume 11, 21; I korinto 2, 5; Efeso 1, 19; 1 Timotheo 1, 14).

-Imani ni zawadi ya Roho Mtakatifu (I korinto 12, 9; Galatia 5, 22). Imani ni mapenzi ya mutu (Matayo 8, 13, ; 9, 22: Makro 5, 34: 10, 52; Luka 7, 50; 17, 19). Imani inakomesha na kuongeza mapenzi ya mutu, ni kusema masikilizano ao mapatano ya mutu na Mungu.

Sababu gani watu wengi wanakataa kumusadiki Mungu?

-Ule mutu anakataa kumusadiki Mungu Yeye ni mufungwa wa mambo na wa vitu vya hii dunia ya bure. Anakataa kumusadiki Mungu kwa sababu Roho yake haimuheshimu Mungu, eko na roho mubaya na ndani yake hakuna imani ya kweli (Yoane 8, 44-46) tena akili yake inajaa na giza sababu anaishi pamoja na shetani mwenye kuondoa maneno ya kweli rohoni mwake.

Kila mutu ana uhuru wa kusadiki ao kukana Yesu Kristu (Luka 16, 23 na Yoane 19, 9 - 10), Wa kusadiki miujiza na kwa malapo yake (Yoane 12, 37 na Zaburi 77, 36).

3) Namna gani mtu anaweza kusadiki Mungu ?

-Mambo ya kwanza mutu kusadiki ni kusikia mahubiri ya imani yenye kutoka katika Mandiko Takatifu (Roma 10, 17) kwa sababu namna gani atasadiki, kama hasikie (Yoane 1, 7; 17, 20, Matendo 8, 12; 14, 27; Roma 1, 5; Efeso 1, 13).

Mambo ya pili ni kusoma Biblia Takatifu, sawa vile ushuhuda moja inasema: «Hii mafundisho yote yameandikwa juu ya kusadiki ya kama Yesu ni Kristu, Mwana wa Mungu na kwa hii imani yenu mupate uzima wa milele katika jina Lake (Yoane 20, 30-31).

Mambo ya tatu ni miujiza ya Mungu «Yoane 6, 30; 7, 31; 11, 23 na 20. 30-31).

Mambo ya ine (4) ni mwangalio wa kiumbe wa Mungu (Roma 1, 20).

Mambo ya tano juu ya mutu kasadiki Mungu ni mahubiri ya mufano na ya uzima wetu wa kweli, ni kusema uzima wetu katika Kristo. Kwa hivi Mtakatifu mmoja anatwaambia: Wewe ukae kimya acha matendo yako ya kuzungumuza».

**MONASTERI YA MTAKATIFU GRIGORIOS**
**KILIMA TAKATIFU**
**GREKIA**
**1996**